# Je, Kwa Nini Kristo Alikufa Msalabani?

# Je, Kwa Nini Kristo Alikufa Msalabani?

John Piper

EDITORIAL PEREGRINO

Je, Kwa Nini Kristo Alikufa Msalabani?

**Editorial Peregrino**
Apartado 19
13350 Moral de Calatrava (Ciudad Real)
Uispania

Kuandaliwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiingereza na Crossway Books, mwaka wa 2006 na kuitwa Fifty Reasons why Jesus came to die.

© 2006 by Desiring God Foundation.

Kuandaliwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiswahili na Editorial Peregrino, mwaka wa 2010

Publication under the auspices of Christian Books Worldwide
© 2010 Editorial Peregrino kwa Kiswahili

Watafsiri: Paul Musembi na Ronald Kogo

Kuhakikishwa na: Sukesh Pabari

Jalada imetayarishwa na Samuel Cabrera Fernandez

Mistari ya Biblia imenuukuliwa kutoka Holy Bible in Kiswahili, © 2009. Imechapishwa na Biblica – Africa, P.O. Box 60595 – 00200, Nairobi, Kenya

Kimechapishwa katika nchi ya Uispania

*Printed in Spain*

# Yaliyomo


1. Kristo alikufa kuondoa ghadhabu ya Mungu. 10
2. Kristo alikufa amfurahishe Mungu Baba. 12
3. Kristo alikufa kujifunza kutii na kukamilishwa. 14
4. Kristo alikufa aweze kupata kufufuka kwake kutoka kwa wafu. 16
5. Kristo alikufa kuonyesha upendo na neema ya Mungu kwa watenda dhambi. 18
6. Kristo alikufa kuonyesha upendo wake kwetu. 20
7. Kristo alikufa ili aifute ile sheria ya Musa ilihitaji kwetu. 22
8. Kristo alikufa ili awe fidia ya wengi. 24
9. Kristo alikufa ili tusamehewe dhambi zetu. 26
10. Kristo alikufa ili tuhesabiwe haki. 28
11. Kristo alikufa ili amalize kutii sheria ili watu wake wawe wenye haki. 30
12. Kristo alikufa ili aondoe hukumu yetu. 32
13. Kristo alikufa ili aonyeshe kutahiriwa na kanuni zingine zote siyo njia ya wokovu. 34

14. Kristo alikufa ili atuokoe na atulinde tuwe waaminifu. 36

15. Kristo alikufa ili atufanye watakatifu, bila lawama na wakamilifu 38

16. Kristo alikufa ili atusafishe dhamira zetu. 40

17. Kristo alikufa ili atupatie kila kitu ambacho ni kizuri kwetu. 42

18. Kristo alikufa ili atuponye kutokana na ugonjwa wa dhambi na ule wa kawaida. 44

19. Kristo alikufa ili awapatie uzima wa milele wote ambao wanamwamini. 46

20. Kristo alikufa ili atuokoe na dunia hii mbovu. 48

21. Kristo alikufa ili atupatanishe na Mungu. 50

22. Kristo alikufa ili atulete kwa Mungu. 52

23. Kristo alikufa ili tuwe mali yake. 54

24. Kristo alikufa ili tuweze kuwa na ujasiri wa kuja kwa Mungu. 56

25. Kristo alikufa ili awe kwetu njia ambayo tunakutana na Mungu. 58

26. Kristo alikufa ili ukuhani wa Agano la Kale ukomeshwe na Yeye awe Kuhani wa milele. 60

27. Kristo alikufa ili awe kuhani mwenye huruma na mwenye usaidizi. 62

28. Kristo alikufa kutukomboa kutokana na mwenendo wa mababu wetu. 64

29. Kristo alikufa kutuondoa kwa utumwa wa dhambi. 66

30. Kristo alikufa ili tuweze kufa kwa dhambi na tuishi kwa utakatifu. 68

31. Kristo alikufa ili tukufe kwa sheria na tuzae matunda kwa Mungu. 70

32. Kristo alikufa ili atuwezeshe kuishi kwa ajili Yake bali siyo kwa ajili yetu. 72

33. Kristo alikufa ili msalaba wake uwe majivuno yetu. 74

34. Kristo alikufa kutuwezesha kuishi kwa imani ndani Yake. 76

35. Kristo alikufa kupatia ndoa maana yake halali. 78

36. Kristo alikufa kuumba watu ambao wako na hamu ya kufanya kazi ya Mungu. 80

37. Kristo alikufa kutuita tufuate mfano wake wa upole na upendo wenye gharama kubwa sana. 82

38. Kristo alikufa kuumba jamii moja ya wafuasi ambao wamejitolea. 84

39. Kristo alikufa kutukomboa kutoka kwa uoga wa kifo. 86

40. Kristo alikufa ili tuweze kuwa naye baada ya kufa kwetu. 88

41. Kristo alikufa kuhakikisha kufufuka kwetu kutoka kwa wafu. 90

42. Kristo alikufa kuzivua enzi na mamlaka. 92

43. Kristo alikufa ili aachilie nguvu za Mungu katika injili. 94

44. Kristo alikufa kuharibu uadui kati ya makabila za ulimwengu. 96

45. Kristo alikufa kuwa fidia ya watu kutoka kila kabila, rangi na taifa. 98

46. Kristo alikufa kukusanya kondoo wake kutoka kila pembe ya ulimwenguni. 100

47. Kristo alikufa kutukomboa kutokana na hukumu wa mwisho. 102

48. Kristo alikufa kupata furaha yake na yetu. 104

49. Kristo alikufa ili aweze kuvikwa taji la utukufu na heshima. 106

50. Kristo alikufa kuonyesha kwamba uovu mbaya sana umekusudiwa na Mungu kwa manufaa ya watu wake. 108

# Je, Kwa Nini Kristo Alikufa Msalabani?

# 1.
# Kristo alikufa kuondoa ghadhabu ya Mungu

*"Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, kwa maana imeandikiwa, 'Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti'" (Wagalatia 3:13).*

*"Yeye ambaye Mungu alimtoa awe dhabihu ya upatanisho kwa njia ya imani katika damu Yake. Alifanya hivi ili kuonyesha haki Yake, kwa sababu kwa ustahimili Wake aliziachilia zile dhambi zilizotangulia kufanywa" (Warumi 3:25).*

*"Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu" (1 Yohana 4:10).*

Neno la Mungu linasema kwamba Mungu huhukumu dhambi. Linatuambia Mungu ni mtakatifu na ni lazima aadhibu wale wafanyao dhambi. Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alikufa msalabani Kalivari. Neno la Mungu pia linatuambia kwamba Mungu ni wa upendo. Hii inamaanisha kwamba Mungu hapendi kizazi chote cha wanadamu kuhukumiwa jahanum. Kwa sababu Mungu ni mtakatifu hataruhusu watenda dhambi kuingia mbinguni. Kwa sababu ya upendo wake, Mungu alimtuma Yesu Kristo afe msalabani Kalivari kwa ajili ya dhambi za watu wake.

Sheria ya Mungu ni wazi. Inasema, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa nguvu zako zote" (Kumbukumbu la Torati 6:5). Lazima sisi wanadamu tutii sheria hii ya Mungu. Lakini ukweli ni kwamba hatumpendi Mungu, bali yake tunapenda vitu vingine kama pesa na anasa za dunia hii. Kwa kufanya hivi tunatenda dhambi dhidi ya Mungu. Hili ni jambo kila mwanadamu amelifanya. Hii ndiyo sababu neno la Mungu linasema, "Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23). Hapa Biblia inazungumza juu ya kila mtu wala si watu fulani pekee.

Kwa hivyo dhambi siyo jambo dogo. Dhambi ni jambo kubwa kwa sababu ni uasi dhidi ya Mungu mwenyewe. Tunapofanya dhambi huwa hatumkosei mwanadamu bali Mungu mwenyewe. Wakati tunakosa kumtii Mungu, huwa tunamkosea heshima na tunajiletea hali ya kukosa furaha.

Biblia inatuambia kwamba Mungu huadhibu dhambi. Hii inamaanisha Mungu hatapuuza dhambi ya mtu yeyote. Mungu hukasirika kwa sababu ya kila dhambi tunayofanya na anaamuru fidia ilipwe kwa kila dhambi tunayofanya. "Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa" (Ezekieli 18:4). Biblia inatuambia wazi kwamba kuna laana juu ya kila mtu mtenda dhambi. Mungu ni mtakatifu na ni msafi. Hawezi akafunga macho yake wakati anaona dhambi ikifanywa. Ni lazima alaani kila dhambi. Biblia inasema kwamba, "Amelaani mtu yule asiyeshika na kutii mambo yote yaliyoandikwa katika kitabu cha sheria" (Wagalatia 3:10; Kumbukumbu la Torati 27:26).

Biblia inatuambia kwamba Mungu ni Mungu ni Mtakatifu na pia ni Mungu wa upendo. Mungu hangekuwa wa upendo, watu wote wangetumwa jahanum. Lakini ukweli ni kwamba Mungu ni Mungu wa upendo na kwa hivyo alimtuma Yesu Kristo aje kutuokoa. Bwana Yesu Kristo alikuja ulimwenguni na akachukua laana ya watu wake: "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kufanyika laana kwa ajili yetu" (Wagalatia 3:13).

Katika mwanzo wa sura hii tumenukuu mstari kutoka kwa kitabu cha Warumi 3:25 ambapo neno "upatanisho" lilitumika. Neno hili linamaanisha kutoa ghadhabu ya Mungu kwa kubandilishana na kitu kingine. Mungu alimtuma Yesu Kristo aje kufa kwa sababu ya watu wake. Wakati alikufa aliitoa ghadhabu ya Mungu ambayo ingeleta hukumu juu ya watu wake.

Ni muhimu sana kwetu wakati tunafikiria kuhusu upendo wa Mungu kuelewa kwamba hayo ni mambo yenye uzito sana. Upendo wa Mungu siyo tu hisia fulani nzuri Mungu ako nazo kwa watu wake. Upendo wa Mungu unadhihirika wakati Mungu mwenyewe alipomtuma Mwanawe aje kufa kwa sababu yetu na kuondoa ghadhabu ya dhambi zetu kutoka kwetu: "Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhami zetu" (1 Yohana 4:10).

# 2. Kristo alikufa amfurahishe Mungu Baba.

*"Lakini yalikuwa ni mapenzi ya Bwana kumchubua na kumsababisha ateseke" (Isaya 53:10).*

*"Mkiishi maisha ya upendo, kama vile Kristo alivyotupenda sisi akajitoa kwa ajili yetu kuwa sadaka yenye harufu nzuri na dhabihu kwa Mungu" (Waefeso 5:2).*

Watu mara mingi hufikiria kwamba nia ya Mungu Baba ni kuwahukumu watu jahanum, Wanafikiria kwamba Mungu Baba hana huruma kamwe na kwamba kama kila kitu kingeachiwa Yeye, basi wanadamu wote wangeangamia jahanum. Na wanaendelea kufikiria kwamba Mungu Baba anataka kuwaadhibu watu wote, lakini Yesu Kristo aliingilia kati na akatuokoa. Kwa mfano, mtoto akikosa na babake atake kumpiga kwa sababu ya makosa ambayo amefanya, mamake mtoto anaingilia kati na kushauriana na baba mtoto ili mtoto asije akapigwa. Baada ya kushauriana na mama mtoto, baba anamua kwamba hatamwaadhibu mtoto. Hivi ndivyo watu wengi wanafikiria kuhusu Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo.

Lakini ni lazima tujue Biblia haisemi kitu kama hicho. Biblia haisemi kwamba nia ya Mungu ni kupeleka watu jahanum. Biblia inafundisha kwamba ni mpango wa Mungu Baba kwamba Bwana Yesu Kristo aje duniani na kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Biblia inatuambia kwamba kabla ya kuumbwa kwa mbingu na aridhi Mungu Baba alipanga wokovu wetu na vile atamtuma Mwanawe duniani kuhakikisha kwamba tunaokolewa. Biblia inasema hivi kuhusu Mungu, "Alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele" (1 Timotheo 1:9).

Tunaposoma Agano la Kale, tunasoma kuhusu mpango huu wa Mungu Baba wa kumtuma Mwanawe duniani afe kwa ajili ya dhambi za watu wake. Nabii Isaya alitabiri mateso na kifo cha Bwana Yesu Kristo. Isaya alisema Kristo, "Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulifikiri amepigwa na Mungu, amepigwa sana naye na kuteswa. Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu...Sisi sote, kama kondoo, tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, naye Bwana aliweka juu yake maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:4-6).

Kifo cha Yesu msalabani Kalivari ulikuwa mpango wa Mungu Baba. Hii ndiyo sababu Agano la Kale linasema, "Lakini yalikuwa ni mapenzi ya Bwana kumchubua na kumsababisha ateseke" (Isaya 53:10).

Hii ndiyo sababu katika Agano Jipya tunasoma kwamba kifo cha Yesu kilimpendeza Mungu Baba. Wakati Kristo alikuwa msalabani, alisema, "Eloi, Eloi, Lama sabakthani? Maana yake, 'Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha'" (Mathayo 27:46). Maneno haya yanamaanisha kwamba Mungu alimwacha Yesu Kristo wakati alikuwa msalabani kwa sababu alimwekelwa dhambi zetu juu yake. Pia Agano Jipya linasema, "Kristo alivyotupenda sisi akajitoa kwa ajili yetu kuwa sadaka yenye harufu nzuri na dhabihu kwa Mungu" (Waefeso 5:2).

Mungu aliimwaga ghadhabu yake juu ya mwanawe na akamwaadhibu kwa sababu ya dhambi zetu. Wakati Yesu alikufa, Mungu Baba alipendezwa na kifo chake, kwa sababu tangu mwanzo alikuwa amepanga hivyo.

# 3.
# Kristo alikufa kujifunza kutii na kukamilishwa

*"Ingawa alikuwa Mwana, alijifunza utii kutokana na mateso aliyoyapata" (Waebrania 5:8).*

*"Ili kuwaleta wana wengi katikautukufu, ilimpendeza Mungu, kwa ajili Yake na kwa kupitia Yeye kila kitu kilichopo, kumkamilisha mwanzilishi wa wokovu wao kwa njia ya mateso" (Waebrania 2:10).*

Katika kitabu cha Waebrania tunaambiwa kwamba Kristo alijifunza kutii kupitia kwa mateso na pia "alifanywa mkamilifu" kupitia kwa mateso. Pia katika kitabu hicho hicho tunaambiwa kwamba Kristo alikuwa bila dhambi: "Yeye mwenyewe alijaribiwa kwa kila namna, kama sisi tujaribiwavyo, lakini Yeye hakutenda dhambi" (Waebrania 4:15).

Hivi ndivyo tunafunzwa katika Biblia kwamba Kristo hakuwa na dhambi kamwe. Tunaambiwa kwamba alikuwa Mwana Mtakatifu wa Mungu. Pia tunaambiwa alikuwa mwanadamu kamili na alipata majaribu na mateso mengi na kupitia mambo mengi magumu kama yale kila mwanadamu anapata katika maisha. Kuna wakati Yesu Kristo alikuwa na njaa (Mathayo 21:18), kuna wakati mwingine Yesu Kristo alikasirika na kuhuzunika (Marko 3:5), na pia kuna wakati mwingine Yesu Kristo alihisi uchungu (Mathayo 17:12). Yesu Kristo alikuwa mwanadamu kamili kama wanadamu wa kawaida, lakini Mungu alimpenda sana kwa upendo mkamilifu: "Yeye hakutenda dhambi, wala udanganyifu haukuonekana kinywani mwake" (1 Petro 2:22).

Kwa hivyo, wakati Biblia inasema kwamba, "alijifunza kutii kupitia mateso," haimaanishi kwamba wakati mwingine Yesu hakuwa akitii na alijifunza kutii baada ya kupitia mateso. Bali inamaanisha kwamba wakati alikuwa akikumbwa na matatizo

alifahamu inamaanisha nini kwa watu wa kawaida kutii neno la Mungu. Wakati tunaambiwa Yesu, "alifanywa mkamilifu kupitia mateso " haimaanishi kwamba hakuwa mkamilifu hadi alipopitia mateso ndiyo akawa mkamilifu. Tunajua kwamba Yesu alikuwa mkamilifu kila wakati. Kile Biblia inasema hapa ni kwamba Yesu Kristo alikuwa anatengeneza hesabu kamilifu ili atuokoe.

Hivi ndivyo ilifanyika wakati Yesu alibatizwa. Hakuhitaji ubatizo kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu. Kwa hivyo alimwambia Yohana, "Kubali hivi sasa; kwa maana ndivyo itupasavyo kwa njia hii kuitimiza haki yote" (Mathayo 3:15).

Hivi ndivyo Biblia inafundisha: Yesu Kristo hangepata majaribu na mateso hapa duniani, hangekuwa mwokozi anayestahili kuwaokoa watu wake. Wakati aliteseka na wakati alipata majaribu alijifunza maana ya kuwa mwanadamu. Ni kama mwanasiasa ambaye amezaliwa katika jamii tajiri na amesomea katika shule mzuri na kuenda katika chuo kikuu ng'ambo. Mtu huyu anaweza kumwambia mtu maskini, "Mimi ni mwanadamu kama wewe," lakini yule maskini anajua kwamba mwanasiasa huyu hawezi kuelewa umaskini ni nini kwa sababu hajawahi kuwa katika hali ya umaskini. Lakini ikiwa ataelewa vyema hali ya kuwa maskini, basi ataweza kumsaidia yule maskini. Jinsi hiyohiyo Yesu alipata mateso na shida mingi ili ajifunze maana ya kuwa mwanadamu anayeishi hapa ulimwenguni. Hivi ndivyo anaweza kuwa mwokozi wetu na anaweza kutuita mandugu na madada (Waebrania 2:17).

# 4.
# Kristo alikufa aweze kupata kufufuka kwake kutoka kwa wafu.

*"Basi Mungu wa amani, ambaye kwa damu ya agano la milele alimleta tena kutoka kwa wafu Bwana wetu Yesu, yule Mchungaji Mkuu wa kondoo, awafanye ninyi wakamilifu mkiwa mmekamilishwa katika kila jambo jeama ili mpate kutenda mapenzi Yake, ili atende ndani yetu kile kinachompendeza machoni Pake, kwa njia ya Yesu Kristo, ambaye utukufu una Yeye milele na milele" (Waebrania 13:20-21).*

*Mungu Baba alipanga kifo cha Bwana Yesu na pia alipanga kufufuka kwake. Hii ndiyo sababu Biblia inasema kwamba Mungu alimleta tena kutoka kwa wafu "Kwa damu ya Agano la milele" (Waebrania 13:20-21).*

"Damu ya Agano la milele" inamaanisha damu ya Yesu Kristo. Yesu alisema, "Hii ndiyo damu yangu ya agano" (Mathayo 26:28). Biblia inatufundisha kwamba ili Yesu atuokoe ilimbidi akufe na afufuke. Yesu hangefufuka, basi hatungeokolewa. Kifo cha Bwana Yesu Kristo kilileta msamaha wa dhambi, kuoshwa kwa dhambi na wokovu kwa watu wa Mungu. Kufufuka kwa Yesu Kristo lilikuwa ni dhihirisho kwamba Mungu Baba amekubali dhabihu yake ya kifo msalabani.

Wakati Yesu alikufa msalabani alijitoa kuwa sadaka kwa watu wake ili awalipie fidia ya dhambi zao. Wakati Mungu Baba alimfufua kutoka kwa wafu lilikuwa dhihirisho kwamba Mungu alifurahishwa na kifo cha Yesu. Mungu Baba alikuwa anasema kwamba kifo cha Yesu kimetosheleza fidia ya dhambi za watu wake.

Biblia inasema, "Kama Kristo hajafufuka, imani yenu ni batili, nanyi bado mko katika dhambi zenu" (1 Wakorintho 15:17). Hii

inamaanisha kwamba kufufuka kwa Yesu Kristo lilikuwa hakikisho kwamba Mungu Baba alikubali kifo cha Yesu Kristo kama malipo yanayokubalika kulipia dhambi za watu wake. Yesu hangefufuka kutoka kwa wafu basi kifo chake hakingemfaidi yeyote. Ni baada tu ya kufufuka ndipo angeweza kuwaokoa watu wake kutoka kwa dhambi zao.

Biblia inasema, "Kristo alifufuka kutoka wafu kwa utukufu wa Baba" (Warumi 6:4). Tukija kwa Yesu Kristo kwa imani na kumwamini yeye pekee kwa wokovu, basi dhambi zetu zitaondolewa na tutasamehewa na kupewa wokovu.

# 5.
# Kristo alikufa kuonyesha upendo na neema ya Mungu kwa watenda dhambi

*"Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Warumi 5:7-8).*

*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).*

*"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake" (Waefeso 1:7).*

Kuna mambo mawili hapa ambayo yanaonyesha kwamba Mungu ako na upendo mkuu kwa wenye dhambi. Kwanza, tunaona upendo mkuu wa Mungu kwa wenye dhambi kwa sababu alimtuma Mwana wake aje kufa kwa ajili yetu: "Alimtoa Mwanawe wa pekee" (Yohana 3:16). Pili, tunaona upendo mkuu wa Mungu kwa wenye dhambi kwa vile sisi tuko wenye dhambi wakuu. Hatukuwa watu wazuri ndipo Yesu aje kukufa kwa sababu yetu, bali tulikuwa wenye dhambi wakuu machoni pa Mungu. Mambo haya mawili yanatuonyesha vile Mungu ako na upendo mkuu kwa sisi wenye dhambi.

Jina "Kristo" linamaanisha mtu muhimu sana, na mtu wa cheo kikuu. Agano la Kale linasema kwamba Kristo ni mfalme wa Waisraeli ambaye analeta amani kwa watu wa Mungu. Pia Agano

la Kale linatueleza kwamba Kristo ni mfalme wa ulimwengu (Isaya 9:6-7).

Mtu yule Mungu alimtuma aje kufa kwa sababu yetu alikuwa mfalme mkuu. Alikuwa Mwana wake mwenyewe. Hii inaonyesha upendo mkuu wa Mungu kwa watu wake.

Watu wale Kristo alikufia walikuwa wenye dhambi. "Yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema - bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu" (Warumi 5:7-8). Tulikuwa wenye dhambi wakuu ambao walistahili kuhukumiwa wala si kuokolewa.

Mungu alimtuma Mwanawe ili afe kwa sababu ya "Wingi wa neema yake" (Waefeso 1:7). Yaani Mungu alimtuma Yesu Kristo kuja duniani ili tupate wokovu bila malipo. Hivi ndivyo upendo wa Mungu ulivyo mkuu, kwamba alimtuma Mwana wake afe kwa ajili yetu na anatupatia wokovu bila malipo.

# 6.
# Kristo alikufa kuonyesha upendo wake kwetu.

*"Mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu na manukato" (Waefeso 5:2).*

*"Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Waefeso 5:25).*

*"Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu" (Wagalatia 2:20).*

Katika kifo cha Bwana Yesu Kristo, Mungu Baba alikuwa anaonyesha upendo mkuu kwa wateule wake (Yohana 3:16). Paulo alijua upendo huu wa Mungu kwake kupitia kwa Kristo Yesu: "Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu" (Wagalatia 2:20).

Wakati tunapofikiria kuhusu msalaba wa Kristo Kalivari, hivi ndivyo tunapaswa kufikiria: kila mtu ambaye ameokoka anapaswa kujua kwamba Kristo alikufa kwa ajili yake. Anapaswa kujua kwamba Kristo anampenda na alikufa kwa sababu yake. Anapaswa kukumbuka kwamba ni dhambi zake mwenyewe zilimtenganisha na Mungu. Anapaswa kukumbuka kwamba hajaokolewa kwa sababu ya mambo mazuri aliyoyafanya lakini ni kwa sababu Yesu Kristo alimhurumia.

Wakati tunawaza juu ya mateso na kifo cha Yesu, tunapaswa kujiuliza swali hili, "Kristo alikufa kwa ajili ya nani?" Jibu kutoka kwa Biblia ni, "Kristo alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Waefeso 5:25). Pia Biblia inaendelea kusema, "Hakuna mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai wake kwa

ajili ya rafiki zake" (Yohana 15:13). Na, "Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi" (Mathayo 20:28).

Biblia inaeleza wazi kwamba Yesu Kristo alikufa kwa sababu ya watu wengi. Swali ambalo kila mtu anapaswa kujiuliza ni, "Je, mimi ni mmojawapo wa wale watakaofaidika na kifo cha Yesu?" Biblia inajibu swali hili hivi, "Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka" (Matendo ya Mitume 16:31); "Kila mtu atakayeliitia Jina la Bwana, ataokoka" (Warumi 10:13); "Kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi katika jina lake" (Matendo ya Mitume 10:43); "Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu" (Yohana 1:12); "Kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

Wakati mtu anasoma maneno haya, Roho Mtakatifu humleta kwa Kristo. Anaona ndani ya Yesu mwokozi aliyekamilika na mtakatifu. Mtu anaona upendo wa Kristo juu yake na anasema,"Kristo alinipenda na akajitoa kwa ajili yangu" (Wagalatia 2:20).

Hii inamaanisha kwamba Kristo alilipa bei kubwa sana na alitununulia zawadi ya bei ghali sana. Hii ndiyo sababu alipokaribia kifo chake aliomba, "Baba, shauku Yangu ni kwamba, wale ulionipa wawe pamoja nami pale nilipo" (Yohana 17:24). Wakati Yesu alikufa msalabani alituonyesha utukufu wa Mungu: "Nasi tukauona utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli" (Yohana 1:14). Tunapoona upendo huu wa Yesu Kristo tunapaswa kuja kwake tukiwa tayari kuwa wafanya kazi wake na kuendelea kuona utukufu wa Mungu kupitia kwake.

# 7.
# Kristo alikufa ili atimize kile sheria ya Musa ilihitaji kwetu.

*"Mlipokuwa wafu katika dhambi zenu na kutokutahiriwa katika asili yenu ya dhambi, Mungu aliwafanya mwe hai pamoja na Kristo. Alitusamehe dhami zetu zote, akiisha kuifuta ile hati yenye mashtaka yaliyokuwa yanatukabili pamoja na amri zake, aliiondoa isiwepo tena, akiigongomea kwenya msalaba Wake" (Wakolosai 2:13-14).*

Watu wengi wanawaza kwamba wakati watakapokufa, Mungu atahesabu ni matendo mazuri mangapi wamefanya na ni matendo mabaya mangapi ambayo wamefanya. Halafu ikiwa matendo mazuri ni mengi sana kuliko matendo mabaya, basi Mungu atawakubali kuingia mbinguni. Hivi ndivyo watu wengi wanavyowaza kuhusu mbinguni. Lakini katika mawazo yao wamejidanganya. Mawazo yao ni ya upuzi kwa sababu:

1. Ni mawazo ya uongo. Watu wengi huwaza kwamba wako na matendo mazuri ambayo wanaweza kumwonyesha Mungu. Lakini ukweli ni kwamba hawana matendo mazuri kwa sababu hayo matendo ambayo wanaita mazuri hawayafanyi kwa kusudi la kumtukuza Mungu. Mungu anataka tufanye matendo mema kwa nguvu na kwa kumtukuza (1 Petro 4:11). Kwa ufupi ni kwamba matendo yetu mazuri lazima yawe na nia moja: kumtukuza Mungu.

Pia kila tendo jema lazima litoke kwa moyo ambao uko na imani. Biblia inasema kwamba, "Cho chote kinachofanywa pasipo na imani ni dhambi" (Warumi 14:23). Watu ambao wanawaza kwamba matendo yao yatawaokoa, wataona kwamba walikuwa wakijindanganya siku ile Bwana Yesu atarudi. "Cho chote sheria inachosema, inawaambia wale walio chini ya sheria ili kila kinywa kinyamazishwe na ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu" (Warumi 3:19). Siku ile Bwana Yesu atarudi, watajua kwamba matendo yao hayastahili chochote kizuri.

2. Hiyo siyo njia ya wokovu. Watu wengi huwaza kwamba matendo mema ni njia ya wokovu, lakini Mungu anakataa. Mtu hawezi kuingia mbinguni kwa sababu ya matendo yake mazuri. Njia moja tu mtu anaweza kuingia mbinguni ni hadi dhambi zake ziwe zimeondolewe na Bwana Yesu Kristo wakati alipokufa msalabani. Huu ndiyo wokovu ambao Biblia inafunza: wokovu kupitia kwa mateso na kifo cha Bwana Yesu Kristo.

Hakuna wokovu katika matendo yako mazuri. Njia moja tu ya kuokolewa, ni dhambi zako ziondolewe kabisa kupitia kwa mateso na kifo cha Bwana Yesu Kristo. Hesabu ya dhambi zetu lazima iondolewe kama tutaingia mbinguni. Hii ndiyo sababu Bwana Yesu Kristo alikufa msalabani.

Wakati Bwana Yesu Kristo alikufa msalabani Kalivari, dhambi zetu ziligongomewa msalabani (Wakolosai 2:13). Kristo mwenyewe alichukua dhambi zetu juu yake. Alifanyika dhambi kwa ajili yetu na akatulipia fidia ambayo sisi tulifaa kulipa. Yeye ndiye tumaini la kila mtenda dhambi na imani ndani yake ndiyo njia ya pekee ya kuokolewa na kuingia mbinguni.

# 8.
# Kristo alikufa ili awe fidia ya wengi.

*"Kwa kuwa hata Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa whai Wake kuwa ukombozi kwa ajili ya wengi" (Marko 10:45).*

Biblia inafunza kwamba wale wote ambao hawajaokoka ni watumwa wa dhambi. Biblia inaendelea kutuambia kwamba njia moja tu ya kuokolewa ni kutolewa kutoka kwa utumwa wa dhambi. Hii haimaanisha kwamba Kristo alimlipa shetani wakati alikufa kwa ajili ya watu wake. Msalabani shetani hakulipwa chochote, bali alishindwa. Bwana Yesu Kristo alikuwa mwanadamu kamili "Ili kwa kifo chake, apate kumwangamiza huyo mwenye nguvu za mauti, yaani, shetiani" (Waebrania 2:14). Msalabani shetani alishindwa.

Wakati Kristo anasema, "Kutoa maisha yangu kuwa fidia ya wengi" (Marko 10:45), anamaanisha kwamba maisha yake ambayo alitoa ndiyo fidia ambayo itawaletea faida wengi.

Labda wewe unajiuliza swali hili, Je, ni nani aliyelipwa fidia hii? Biblia inasema kwamba fidia hii ililipwa kwa Mungu. Biblia inasema, "Kristo alivyotupenda sisi akajitoa kwa ajili yetu kuwa sadaka yenye harufu nzuri na dhaihu kwa Mungu" (Waefeso 5:2). "Basi si zaidi sana damu ya Kristo, ambaye kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo waa kutusafisha dhamira zetu" (Waebrania 9:14). Ilimbidi Kristo afe kwa ajili yetu kwa sababu tulitenda dhambi dhidi ya Mungu na kupungukiwa na utukufu wake (Warumi 3:23). Ni kwa sababu ya dhambi zetu, ulimwengu wote uko chini ya hukumu ya Mungu (Warumi 3:19). Kwa hivyo wakati Kristo alipojitoa kuwa fidia yetu, Biblia inasema kwamba tumewekwa huru kutokana na hukumu ya Mungu. "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu" (Warumi 8:1). Sisi sote tunahitaji kuondolewa katika hukumu ya mwisho ya Mungu (Warumi 2:2; Ufunuo 14:7).

Kwa hivyo Kristo alikufa kuwa fidia ili tuweze kuondolewa katika hukumu ya Mungu. Hii ndiyo sababu Kristo aliwaambia wanafunzi wake mara kwa mara, “Mwana wa Adamu atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa watu nao watamwua” (Marko 9:31). Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alijiita, “Mwana wa Adamu.” Mungu hawezi kufa, lakini mwanadamu hufa. Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, hii ndiyo sababu alikuwa mwanadamu.

Biblia ni wazi kwamba Yesu hakulazimishwa kufa msalabani. Kristo mwenyewe anasema kwamba, “Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa bali kutumika” (Marko 10:45). Alijitolea kuwa mtumishi wetu na alijitolea kufa kwa ajili yetu. Ndiyo sababu anasema, “Hakuna mtu aniondoleaye uhai wangu, bali ninautoa kwa hiari yangu mwenyewe” (Yohana 10:18). Sababu ya Yeye kutoa maisha yake kwa ajili ya watu wake, ni kwa sababu ya upendo juu yao. Alichagua kufa kwa ajili yao kwa sababu aliwapenda.

Je, ni watu wangapi ambao Kristo alikufia msalabani? Alisema kwamba, “Alikuja kutoa maisha yake kuwa fidia ya wengi.” Wengi haimaanishi wote. Siyo kila mtu ataokoka; lakini watu wote wamealikwa kuja kwake ili waokolewe: “Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani, mwanadamu Kristo Yesu, aliyejitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wanadamu wote”(1 Timotheo 2:5-6).

# 9.
# Kristo alikufa ili tusamehewe dhambi zetu

*"Katika Yeye tunao ukombozi kwa njia ya damu Yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neeme Yake" (Waefeso 1:7).*

*"Hii ndiyo damu yangu ya agano, ile imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi" (Mathayo 26:28).*

Kwa kawaida mtu akitukosea, mara mingi sisi huwasamehe na huwa hatulipizi kitendo kilichotendwa dhidi yetu. Kwa mfano, mtoto akiharibu simu ya babake halafu babake amsamehe, baba huwa hatarajii mtoto kulipa simu yake. Baba akimwambia mtoto, "nimekusamehe," anamaanisha ya kwamba mtoto amekosea lakini amemsamehe.

Hivi ndivyo Mungu hutusamehe ikiwa tutamwamini mwanawe Yesu Kristo na tuweze kukombolewa: "Kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi katika jina lake" (Matendo ya Mitume 10:43). Tunapokombolewa kupitia kwa Yesu Kristo, Mungu anatusamehe dhambi zetu zote. Hivi ndivyo Bibilia inavyosema: "Mimi ndimi nizifutaye dhambi zako, kwa ajili yangu mwenyewe" (Isaya 43:25); "Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo Mungu ameziweka dhambi zetu mbali na sisi" (Zaburi 103:12).

Tunafaa tuelewe kwamba kabla Mungu asamehe mtu inapaswa kuwa na fidia ambaye amelipwa. Ni kama mtu ambaye ameua mwingine na baadaye kumwambia hakimu, "Pole, nimeua mtu, tafadhali nisamehe." Hakimu hawezi kumwachalia aende. Amemwua mtu na lazima aadhibiwe hata kama anasema pole.

Hivi ndivyo ilivyo na kila mtenda dhambi; ni lazima aadhibiwe kwa sababu ya dhambi zake. Dhambi zote ni mbaya kwa sababu ni uasi dhidi ya Mungu mwenyewe.

Hii ndiyo sababu Yesu aliteswa na akafa: "Kwa damu yake tunao ukombozi na msamaha wa dhambi" (Waefeso 1:7) Tunapoenda kwa Yesu kwa kumwomba msamaha, tunasamehewa kwa sababu Yesu amezilipia dhambi zetu. Msamaha ni zawadi ya bure kwetu kutoka kwa Mungu kwa sababu Yesu alitununulia zawadi hii.

# 10.
# Kristo alikufa ili tuhesabiwe haki.

*"Basi, kwa kuwa sasa tumehesabiwa haki katika damu yake" (Warumi 5:9).*

*"Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu" (Warumi 3:24).*

*"Mwanadamu huhesabiwa haki kwa njia ya imani wala si kwa matendo ya sheria" (Warumi 3:28).*

Mtu ambaye ako huru ni mtu ambaye amesamehewa dhambi zake zote. Kwa mfano, mtu akipelekwa kotini ili ahukumiwe. Kotini hakimu husikiza mashtaka ya mtu huyu na ushuhuda. Halafu baada ya kusikiza, anasema ushuhuda siyo dhabiti, huyu mtu hana makosa na yuko huru kwenda.

Kufanywa huru ni kitu ambacho hutendeka katika mahakama ya sheria. Hakimu anaposema hana makosa anamaanisha mtu huyo hawezi kuendelea kuzuiliwa gerezani.

Bibilia inatufundisha ya kuwa wakati Mungu anatuokoa, yeye huwa anatusamehea dhambi zetu zote. Hii inamaanisha ya kuwa yeye huhakikisha kwamba sisi ni wasafi mbele yake.

Katika mahakama ya sheria, ikiwa mtu anaachiliwa huru inamaanisha kwamba hana hatia yoyote ijapokuwa aliwekelewa mashtaka. Hakimu atapata ya kuwa hana hatia yoyote. Hii inamaana ya kuwa mtu huyu hakukeuka sheria kwa njia yoyote ile.

Lakini mbele ya macho za Bwana sisi wote ni wenye dhambi, tumekeuka sheria za Bwana. Kwa hivyo hatuwezi linganishwa na yule mtu aliye katika mahakama ya kisheria. Bibilia inasema ya kwamba, "Yeye asemaye asiye haki ana haki, naye asemaye mwneye haki hana haki, Bwana huwachukia sana wote wawili"

(Mithali 17:15). Na Mungu huwaweka huru wanawo mwamini (Warumi 4:5). Kwa maneno mengine Mungu hufanya maajabu.

Bibilia inatuambia kwamba Mungu huchukua mtu mwenye dhambi kotini mwake na kumtangaza mwenye haki. Hii ni kwa sababu mtu huyu amemwamini Yesu Kristo na ameokolewa. “Na kwa hivyo Mungu anaweza kuwa mfanya haki kwa yule ambaye anayeamini Yesu” (Warumi 3:26). Kuna sababu mbili kwa nini Mungu anaweza kufanya hivi. Kwanza ni kwa sababu Yesu alikufa kulipa deni kwa ajili ya kila mtu atakayemwamini. “Tumehesabiwa haki kwa damu yake” (Warumi 5:9). Mtu huja kotini kama ana makosa. Ameishi maisha ya dhambi. Yesu atachukua rekodi hii ya dhambi na kulipa deni yake. Hii ndiyo sababu Mungu humtangaza mtu huru.

Sababu ya pili tutaangalia katika ukurasa unaofuatia.

# 11.
# Kristo alikufa ili amalize kutii sheria ili watu wake wawe wenye haki.

*"Akiwa na umbo la wanadamu, alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba" (Wafilipi 2:8).*

*"Kwa maana, kama vile kwakutotii yule mtu mmoja, wengi walifanywa wenye dhambi, vivyo hivyo, kwa kutii kwa mtu mmoja, wengi watafanywa wenye haki" (Warumi 5:19).*

*"Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye" (2 Wakorintho 5:21).*

*"Nionekane mbele Zake nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu kwa njia ya imani" (Wafilipi 3:9).*

Wakati Mungu anamwokoa mtu anafanya mambo mawili. Kwanza anaondoa dhambi za mtu huyu. Pili anampatia mtu huyu haki ambayo inatokana na Kristo. Hii ndiyo sababu tunaweza kusema, "Nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani katika Kristo" (Wafilipi 3:9).

Tunapewa haki itokanayo na Kristo. Hii inamaanisha kwamba Bwana Yesu Kristo alitii sheria ya Mungu kikamilifu. Kwa hivyo wakati tunamwamini, anatupatia utiifu wake. Kwa njia hii tunahesabiwa wenye haki. Wakati Mungu anatutazama, haoni hesabu yetu ya dhambi, bali anaona haki ambayo hutokana na Kristo Yesu.

Hivi ndivyo Mungu anavyomhesabu haki mwenye dhambi (Warumi 4:5). Kwanza kabisa kifo cha Kristo kililipia dhambi zetu halafu tunapewa utiifu wake Kristo Yesu na katika mahakama ya Mungu tunahesabiwa wenye haki. Hivi ndivyo tunavyohesabiwa haki.

Mateso na kifo cha Bwana Yesu Kristo ndiyo msingi wa wokovu wetu. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu" (Isaya 53:5). Kifo chake msalabani kilikuwa kitendo cha utiifu kwa Mungu Baba. Katika maisha yake yote alimtii Babake na kwa kifo chake alikamilisha utiifu wake: "Alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba (Wafilipi 2:8). Kwa sababu alitii, tutaingia mbinguni. "Kwa kutii kwa mtu mmoja, wengi watafanywa wenye haki" (Warumi 5:19).

Kwa hivyo ni kifo na mateso ya Kristo ndiyo msingi wa wokovu wetu. "Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye" (2 Wakorintho 5:21). Wakati Biblia inasema kwamba alifanyika dhambi kwa ajili yetu, inamaanisha kwamba dhambi zetu ziliwekwa juu yake na tumesamehewa kwa sababu alikufa kwa ajili yetu. Papo hapo tulipewa haki yake ili tuwe wenye haki machoni pa Mungu.

Kwa hivyo ndani ya Yesu kuna wokovu kamili: yaani dhambi zetu zimeondolewa na tumepewa haki yake. Haya yote tunayapokea kwa imani.

# 12.
# Kristo alikufa ili aondoe hukumu yetu.

*"Ni nani basi atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, zaidi ya hayo, ndiye aliyefufuka katika wafu, yuko mkono wa kuume wa Mungu; naye ndiye anayetuombea" (Warumi 8:34).*

Kwa sababu Bwana Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya watu wake, Biblia hivi ndivyo inazungumza kuhusu wale ambao wameokoka: "Sasa, hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu" (Warumi 8:1). Kuokoka inamaanisha kuwa katika ushirika na Kristo Yesu kwa imani. Wakati tunaokolewa tunaungana na Kristo Yesu. Tunaungana naye katika mateso na kifo chake, na kifo chake kinakuwa wokovu wetu.

Hii inamaanisha kwamba njia moja tu tunaweza kuokolewa, ni kwa imani ndani ya Kristo Yesu. Imani inatuleta kwa Kristo Yesu na haki yake inakuwa yetu. Mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ndani ya Kristo Yesu. Sisi tulimwamini Kristo Yesu ndipo tukahesabiwa mwenye haki na wala si kwa matendo ya sheria; "Mtu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria bali kwa njia ya imani katika Yesu Kristo" (Wagalatia 2:16). "Kuhesabiwa haki kwa imani" na "kuhesabiwa haki katikaKristo" (Wagalatia 2:17), yote mawili yanamaanishi kitu kimoja. Tuko ndani ya Kristo kwa imani na kwa hivyo tunahesabiwa wenye haki.

Wakati tunaokolewa kwa imani ndani ya Kristo, hatutahukumiwa; kifo chake kinatuondoa katika hukumu ya Mungu. Wakati tunakuja kwake kwa imani, tunahakikishiwa wokovu wetu kuwa ni wa milele.

Hii haimaanishi kwamba maisha ya ukristo ni rahisi na ni bila matatizo. Hata kama tunaondolewa katika hukumu ya Mungu, ulimwengu bado unatuchukia sana. Ulimwengu utajaribu

kutushitaki. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, “Ni nani atakayewashtaki wale ambao Mungu amewachagua? Ni Mungu mwenye ndiye mwenye kuwahesabia haki” (Warumi 8:33). Tena Biblia inasema, “Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni shida au taabu au mateso au njaa,au uchi au hatari au upanga?” (Warumi 8:35). Jibu ni kwamba hakuna chochote kwa vitu hivi ambacho kinaweza kututenganisha na Mungu. Lakini katika mambo hayo yote, “Tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda” (Warumi 8:37).

Mara mingi ulimwengu utatuchukia sana na mara mingi wakristo watakufa kwa ajili ya imani yao. Lakini hata wakifa wako na ahadi hii kutoka kwa Mungu: “Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani awezaye kuwa kinyme chetu?” (Warumi 8:31). Hata kama ulimwengu unatuchukia, tusife moyo. Sisi ni wenye haki machoni pa Mungu kupitia kwa imani ndani ya Kristo Yesu. Kristo alikufa kwa ajili yetu na Kristo amefufuliwa kutoka kwa wafu kwa ajili yetu. Sisi tuko hai ndani mwake na hakuna hukumu kwetu. “Wenye haki ni wajasiri kama simba” (Mithali 28:1).

# 13.
# Kristo alikufa ili aonyeshe kwamba kutahiriwa na kanuni zingine zote siyo njia ya wokovu.

*"Ndugu zangu, kama mimi bado ninahubiri kuhusu kutahiriwa, kwa nini basi niteswe na Wayahudi? Ukweli kwamba bado wananitesa, ni ushahidi kwamba bado ninahubiri wokovu kupitia msalaba wa Kristo peke yake"*
*(Wagalatia 5:11).*

*"Wale wanaotaka kuonekana wazuri kwa mambo ya mwili wanaotaka wawalazimishe kutahiriwa, sababu pekee ya kufanya hivyo ni kuepuka kuteswa kwa ajili ya msalaba wa Kristo"*
*(Wagalatia 6:12).*

Katika kanisa la Agano Jipya kulikuwa na upinzani mkubwa kuhusu kutahiriwa. Katika Mwanzo 17:10 Mungu aliamrisha kutahiriwa kwa Wayahudi. Bwana Yesu alikuwa Myahudi, na pia watume wote kumi na wawili. Na kwa hivyo kanisa lilipozaliwa katika Agano Jipya utamaduni wa kutahiriwa uliingia na kusababisha kuchanganyikiwa kwingi na mabishano.

Shida ya kwanza iliingia wakati watu wasiokuwa Wayahudi walipookoka. Halafu iliwabidi wakristo wachunguze utamaduni wa kutahiriwa. Je, mtu akitaka kuokoka, lazima atahiriwe au wokovu ulikuwa kwa imani pekee ndani ya Kristo pekee? Hili ndilo swali ambalo walijiuliza.

Wakati mitume walienda kuhubiri kwa watu ambao hawakuwa Wayahudi, ujumbe wao ulikuwa wazi. Petro alihubiri, "Kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi katika jina lake" (Matendo ya Mitume 10:43).

Kwa hivyo mitume walihubiri wazi: wokovu ni kwa imani pekee na sio kwa kutahiriwa au kitu chochote kama hicho. Lakini, katika kanisa la kwanza kulikuwa na wakristo wengine ambao walikuwa wamechanganyikiwa kuhusu jambo hili. "Baadhi ya watu wakashuka Antiokia kutoka Uyahudi, nao wakawa wanawafundisha ndugu walioamini kwamba, 'Isipokuwa mmetahiriwa kufuatana na desturi aliyofundisha Mose, hamwezi kuokoka" (Matendo Ya Mitume 15:1).

Wakristo wa hiyo siku walikutana pamoja kujadili kuhusu jambo hili: "Ndipo baadhi ya walioamini wa madhehu ya Mafarisayo wakasimama na kusema, 'Hao watu Mataifa lazima watahiriwe na waagizwe kuzitii sheria za Mose. Mitume na wazee wakakutana pamoja ili kufikiri jambo hili. Baada ya majadiliano mengi, Petro akasimama na kusema, 'Ndugu zangu, mnajua kwamba siku za kwanza Mungu alinichagua ili kwa mdomo yangu watu Matifa wapate kusikia ujumbe wa injili na kuamini. Mungu, yeye ajuaye mioyo alionyesha kwamba anawakubali kwa kuwapa Roho Mtakatifu kama vile alivyotupa sisi. Mungu hakutofautisha kati yetu na wao, bali alitakasa mioyo yao kwa imani. Sasa basi, mbona mnataka kumjaribu Mungu kwa kuweka kongwa shingoni mwa wanafunzi ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulibeba? Lakini sisi tunaamini ya kuwa tunaokolewa kwa neema ya Bwana Yesu Kristo, kama wao wanavyookolewa. Kusanyiko lote litakaa kimya, wakawasikiliza Paulo na Barnaa wakieleza jinsi Mungu alivyowatumia kutenda ishara na maajabu kwa watu mataifa" (Matendo Ya Mitume 15:5-12)

Paulo aliona jambo hilo wazi kabisa. Aliona kwamba ikiwa watu watalazimishwa kutahiriwa ili wapate wokovu, basi kifo cha Kristo kilikuwa bila faida. Paulo alisema ikiwa tunawaza kwamba kutahiriwa kunatuokoa basi msalaba wa Kristo hauna maana kwetu Msalaba wa Kristo unatuweka huru sisi kutoka kwa matendo yote ya wanadamu kama hayo: "Kristo alitupa uhuru, akataka tubaki huru. Hivyo simameni imara wala msikubali tena kulemewa na kongwa la utumwa" (Wagalatia 5:1).

# 14.
# Kristo alikufa ili atuokoe na atulinde tuwe waaminifu.

*"Hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi" (Marko 14:24).*

*"Nitafanya nao agano la milele: Kamwe sitaacha kuwatenda mema; nami nitawavuvia kuniacha mimi, ili kwamba kamwe wasigeukie mbali nami" (Yeremia 32:40).*

Biblia inazungumza kuhusu "Agano la Kale" na "Agano Jipya". Neno Agano linamaanisha makubaliano kati ya watu wawili ambayo hayafai kuvunjwa. Katika Agano hili watu wote wawili wana majukumu ambayo ni lazima wayatimize. Katika Bibilia Mungu ameweka maagano na mwanadamu na katika maagano hayo Mungu anaahidi mambo fulani na mwanadamu ako na majukumu ya kutimiza.

"Agano la kale" ni lile Agano ambalo Mungu alifanya na taifa la Israeli kupitia Musa wakati alipopeana Amri Kumi. Kwa sababu moyo wa mwanadamu ni moyo wenye dhambi, Waisreali hawakuweza kuzitimiza sheria za Mungu. Kwa sababu ya hii Mungu alituma manabii ambao walizungumza kuhusu Agano Jipya. Walisema siku itakuja wakati Mungu atafanya Agano Jipya na watu wake, "Si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha" (2 Wakorintho 3:6)

Mateso na kifo cha Bwana Yesu Kristo ndiyo msingi wa Agano Jipya: "Kwa sababu hii Kristo ni mjumber wa agano jipya" (Waebrania 9:15). Yesu alisema kwamba damu yake ilikuwa ya, "Agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi" (Marko 14:24). Hii inamaanisha kwamba damu ya Yesu huleta baraka za Agano Jipya kwa watu wake.

Katika Agano la Kale nabii Yeremia aliongea kuhusu Agano Jipya. Mungu alisema, "'Wakati unakuja,' anasema Bwana, 'nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. Halitafanana na agano nililofanya na baba zao wakati nilipowashika mkono na kuwaongoza watoke Misri, kwa sababu walivunja agano langu, ijapokuwa nilikuwa mume kwao,' asema Bwana. Hili ndilo agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya wakati ule,' asema Bwana. Nitaweka sheria yangu ndani yao na kuiandika katika mioyo yao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watoto wangu. Mtu hatamfundisha tena jirani yake, au mtu kumfundisha ndugu yake akisema, 'Umjue Bwana Mungu,' kwa sababu wote watanijua mimi, kuanzia aliye mdogo kabisa kwao hata aliye mkuu sana.' asema Bwana. Kwa sababu nitausamehe uovu wao na sitazikumbuka dhambi zao tena" (Yeremia 31:31-34). Kwa sababu Bwana Yesu alikufa kwa ajili ya watu wake, sisi tumeokolewa na sasa tuna baraka nyingi: Mungu hubadilisha mioyo yetu wakati anatuokoa

Agano Jipya haliwezi kukosa kufaulu kwa sababu Kristo hulihakikisha. Kristo huwapa imani watu wake na huwadumisha ili wawe waaminifu kwake. Yeye huwaokoa watu wake kutoka dhambi zao na huandika sheria zake kwenye mioyo yao, kwa sababu katika Agano Jipya "Roho huhuisha" (2 Wakorintho 3:6). "Hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu; alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu" (Waefeso 2:5). Mungu anapotuokoa hutupatia maisha ya kiroho ili sisi tuje kwa Kristo kwa imani. Katika njia hii Kristo anawaita watu wake kutoka kila mahali ulimwenguni mwote.

Kwa hivyo Mungu anapotuokoa hutupatia imani. Lakini mara tunapookoka, yeye huhakikisha kwamba hatuondoki kutoka kwake na kupoteza wokovu wetu. "Nitafanya nao agano la milele: Kamwe sitaacha kuwatendea mema, nami nitawavuvia kuniacha mimi, ili kwamba kamwe wasigeukie mbali nami" (Yeremia 32:40). Wakati Yesu alikufa alihakikisha kwamba tutasamehewa na kwamba tutakuwa na uzima wa milele pamoja naye mbinguni. Yeye hataturuhusu sisi kumwacha yeye na tupoteze wokovu wetu, atatudumisha sisi katika uaminifu.

# 15.
# Kristo alikufa ili atufanye watakatifu, bila lawama na wakamilifu

*“Kwa sababu kwa dhabihu moja amewafanya kuwa wakamilifu milele wale wote wanaotakaswa” (Waebrania 10:14).*

*“Lakini sasa Mungu amewapatanisha ninyi kwa njia ya mwili wa Kristo kwa kupatia mauti, ili awalete mbele Zake mkiwa watakatifu, bila dosari wala lawama” (Wakolosai 1:22).*

*“Ondoeni chachu ya kale ili mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Kristo, Mwana-Kondoo wetu wa Pasaka amekwisha tolewa kuwa dhabihu” (1 Wakorintho 5:7).*

Jambo moja ambalo linawashusha mioyo wakristo ni jinsi wanavyokuwa polepole katika ukristo wao. Wanajua kwamba Mungu amewaita wampende kwa mioyo yao yote na kwa nafsi yao yote na kwa akili zao zote na kwa nguvu zao zote (Marko 12:30). Lakini wanapata kwamba katika maisha haya hawawezi kumpenda Mungu kabisa. Mara mingi wanajipata wakisema, “Ole wangu, mimi maskini! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?” (Warumi 7:24). Wanajua kwamba Mungu anawaamrisha wawe wakamilifu, na pia kwamba wawo siyo wakamilifu: “Si kwamba nimekwisha kufika, au kwamba nimekwisha kuwa mkamilifu; la hasha! Bali nakaza mwendo ili nipate kile ambacho kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu” (Wafilipi 3:12).

Biblia inasema, “Nimeshikwa na Kristo Yesu.” Hii inatueleza ni kwa sababu gani ni lazima tuwe watakatifu. Siyo kwamba wakati tunakuwa watakatifu ndipo Kristo anatukubali kuwa watu wake. Katika mstari huu Paulo anasema kwamba, Yesu Kristo

amenifanya tuwe wake. Sisi ni wake tayari, hatufanyiki wake wakati tunajitahidi kuwa watakatifu. Tunajitahidi kuwa watakatifu kwa sababu sisi ni wake tayari.

Biblia inaendelea kutueleza kwamba hata wakati tunajitahidi kuwa watakatifu, machoni pa Mungu sisi ni watakatifu tayari. Biblia inasema, “Kwa sababu kwa dhabihu moja amewafanya kuwa wakamilifu milele wale wote wanaotakaswa” (Waebrania 10:14). Kwa hivyo katika msitari huu tunaambiwa kwamba tayari tumekamilishwa.

Biblia inafunza jambo hili wakati inasema kwamba tuondoe chachu wa dhambi maishani mwetu. “Ondoeni chachu ya kale ili mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Kristo, Mwana-Kondoo wetu wa Pasaka amekwisha tolewa kuwa dhabihu” (1 Wakorintho 5:7). Tena katika mstari huu tunaambiwa kwa sababu Kristo, Mwana-kondoo wa pasaka ametolewa kama sadaka, kifo chake kinatukamilisha. Kwa hivyo tunahitajika kupigana ili tuondoe uchafu wote miongoni mwetu. Sisi ndiyo watoto wakamilifu wa Mungu kwa hivyo inatupaswa kuishi maisha matakatifu.

# 16.
# Kristo alikufa ili atusafishe dhamira zetu

*"Basi si zaidi sana damu ya Kristo, ambaye kwa Roho wa milele alijitoa nafsi Yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na waa kutusafisha dhamiri zetu, kutokana na matendo yaletayo mauti, ili tupate kumtumikia Mungu aliye hai!" (Waebrania 9:14).*

Wakati Adamu na Hawa walipoanguka katika dhambi, walifanyika wenye dhambi na wenye hatia. Dhambi yao iliharibu kila kitu na walijua jambo hili na kwa hivyo walishikwa na aibu. Dhambi yao iliharibu ushirika wao na Mungu, ndiyo sababu walijificha kutoka kwake. Dhambi hiyo iliharibu uhusiano wao wawili ndiyo sababu walianza kulaumiana. Pia dhambi yao iliharibu amani ambayo walikuwa nayo na wakawa na aibu.

Watu wa Mungu katika Agano la Kale walikuwa na shida hii wote. Walijua kwamba wametenda dhambi dhidi ya Mungu na dhamira yao iliwahukumu. Sadaka za wanyama ambazo walikuwa wakileta hekaluni hazikuondoa hatia ya dhamira zao. "Huu ulikuwa mfano kwa ajili ya wakati wa sasa, kuonyesha kwamba sadaka na dhabihu zilizokuwa zikitolewa hazikuweza kusafisha dhamiri ya mtu anayeabudu. Lakini hizi zilishughulika tu na vyakula na vinywaji pamoja na taratibu mbalmbali za kunawa za nje, kanuni kwa ajili mwili zilizowekwa hadi wakati utimie wa matengenezo mapya" (Waebrania 9:9-10). Wanyama ambao waliletwa kama sadaka katika hekalu waliosha tu nje ya mwili lakini siyo dhamira.

Hakuna damu ya mnyama ambayo ingeweza kuosha dhamira, na watu walielewa jambo hili (Isaya 53 na Zaburi 51). Hili ni jambo ambalo hata sisi tunajua: damu ya mnyama haiwezi kutupatia amani na Mungu. Hii ndiyo sababu Bwana Yesu Kristo alikuja kuwa kuhani mkuu zaidi. Alileta sadaka bora zaidi: siyo mnyama bali Yeye mwenyewe. "Basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa

sadaka isiyo kuwa na mawaa, itawasafisha dhamira zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai (Waebrania 9:14). Kifo cha Bwana Yesu Kristo kinatuletea wokovu kwa kila mtu ambaye anamwamini. Hata watu wa Agano la Kale waliokolewa kupitia kwa kifo chake.

Hata leo shida ya mwanadamu ni ile ile: tunajua kwamba tumetenda dhambi dhidi ya Mungu na dhamira zetu hazina amani. Tunajihisi kwamba hatuna uzuri wowote kuja kwa Mungu.

Kuna watu wengi ambao hujaribu kufanya matendo mengi mazuri kwa tumaini kwamba matendo yao mazuri yatawawezesha kuja mbele za Mungu. Lakini hata baada ya kufanya matendo haya, bado wanajihisi kwamba dhambi zao haziwaruhusu kuwa katika ushirika na Mungu; dhamira zao haziwaletei amani. Yesu alisema kile ambacho kinatoka katika mwanadamu ndiyo kinacho mfanya awe mwenye dhambi (Marko 7:15-23). Ni kiburi chetu na tamaa zetu na hasira zetu na uchungu wetu, mambo haya ndiyo yanatufanya kuwa watenda dhambi. Haya yote ni mambo ambayo yanatoka katika moyo wenye dhambi na yanaitwa matendo mafu kwa sababu yanatoka katika moyo ambao umekufa kwa Mungu na hauna maisha ndani mwake.

Dawa kwa dhamira ambayo inasumbuka ni damu ya Kristo Yesu. Wakati tunakuja kwa Kristo Yesu, damu yake inatuosha kutokana na dhamira chafu na kutuleta katika amani na Mungu. Ndiyo njia ya pekee tunaweza kuwa na amani na ushirika na Mungu.

# 17.
# Kristo alikufa ili atupatie kila kitu ambacho ni kizuri kwetu

*"Ikiwa Mungu hakumhurumia Mwanawe, gali alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosage basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja Naye?" (Warumi 8:32).*

Katika mstari huu, tunaambiwa kwamba mahitaji yetu yote yanapeanwa katika Kristo Yesu. Kile Biblia inasema ni: Mungu ametupatia zawadi kuu ambayo ni Mwanawe. Je, atawezaje kukosa kutupatia mambo mengine ambayo ni ya manufaa kwetu? Ikiwa ametupatia kile ambacho ni cha muhimu sana, basi hawezi kukosa kutupatia mambo ambayo ni madogo.

Kile mstari huu unafunza ni kwamba Mungu hatatunyima chochote ambacho anajua kwamba ni kizuri kwetu. Ikiwa anajua kwamba kuna kitu ambacho kitakuwa cha manufaa kwa maisha yako ya kiroho, basi atapeana kitu hicho.

Swali ambalo tunafaa kujiuliza ni, "Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kila kitu?" Biblia haimaanishi kwamba Mungu atatupatia maisha yenye starehe hapa ulimwenguni. Pia haimaanishi kwamba hatutakuwa na maadui. Tunajua hivi kwa sababu katika kifungu hicho hicho Paulo anasema, "Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa, tunahesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa" (Warumi 8:36). Kuna wakristo wengi katika ulimwengu leo ambao wanapitia mambo magumu sana ambayo yanasababishwa na maadui wa Mungu. Lakini wanafaa kuhimizwa kutokana maneno haya, "Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je, ni shida au taabu au mateso au njaa au uchi au hatari au upanga?" (Warumi 8:35). Biblia inazungumza kuhusu mambo haya yote katika mstari huu kwa sababu Mungu anajua kwamba mambo haya yatawafikia wakristo wote. Tunakumbana na majaribu haya, "Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, naam na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda" (Warumi 8:37).

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba kwa sababu ya kifo cha Bwana Yesu Kristo, Mungu atatupatia kila kitu? Inamaanisha kwamba Mungu atatupatia kila kitu ambacho ni kizuri kwetu. Inamaanisha kwamba atatupatia kila kitu ambacho kitatusaidia kukamilika katika mfano wa Kristo Yesu (Warumi 8:29). Inamaanisha kwamba atatupatia kile ambacho kitatuwezesha kuingia mbinguni.

Biblia inatufunza jambo hili wazi wakati inasema, "Naye Mungu wangu atawajaza ninyi kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri Wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 4:19). Katika kifungu hicho hicho tunasoma, "Ninajua kupungukiwa, pia ninajua kuwa vingi. Nimejifunza siri ya kuridhika katika kila hali, wakati wa kushiba na wakati wa kuona njaa, wakati wakuwa na vingi na wakati kupungukiwa. Naweza kuyafanya mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:12-13).

Paulo katika kifungu hiki anasema kwamba anaweza kufanya kila kitu katika Kristo. Kuwa mwangalifu sana kwa sababu katika maneno haya anazungumza kuhusu kuvumilia katika kila hali, kama hali ya njaa au wakati ako na hitaji lolote. Kwa maneno haya anamaanisha Mungu atatosheleza kila hali kwa mapenzi yake. Hiyo haimaanishi kwamba atatupatia chakula, mavazi, afya njema, na utajiri kila wakati. Bali inamaanisha kwamba atatuwezesha kuvumilia wakati wa njaa, umaskini na wakati tuko na hitaji lolote ambalo tunaweza kuwa nalo. Kupitia kwa mateso na kifo cha Bwana Yesu Kristo, Mungu atatupatia kila kitu ambacho kitamletea utukufu.

# 18.
# Kristo alikufa ili atuponye kutokana na ugonjwa wa dhambi na ule wa kawaida

*"Adhabu iliyotuletea sis amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona" (Isaya 53:5).*

*"Jioni ile, wakamletea watu wengi waliopagwa na peop, naye akawatoa wale pepo kwa neno lake, na kuponya wagonjwa wote" (Mathayo 8:16).*

Kwa sababu Bwana Yesu Kristo aliteswa na kufa, siku moja ugonjwa wote utaisha katika ulimwengu. Wakati Mungu alipoumba ulimwengu hakukuwa na kifo au magonjwa, yote yalikuja kwa sababu ya hukumu wa Mungu ambao ulikuja kwa sababu ya dhambi ya Adamu. Biblia inasema, kwa maana "Viumbe vyote viliwekwa chini ya ubatili, si kwa chaguo lao, bali kwa mapenzi Yake Yeye aliyecitiisha katika tumaini" (Warumi 8:20). Mungu alihukumu ulimwengu kuonyesha kwamba dhambi ni kitu hatari sana.

Kwa kuanguka kwa mwanadamu, kifo kiliingia ulimwenguni: "Kwa hiyo, kama vile dhambi ilivyoingia ulimwenguni kupitia dhambi hii, mauti ikawafikia watu wote" (Warumi 5:12). Pia Biblia inatuambia kwamba matokeo ya dhambi yanawadhuru hata wale ambao wameokoka: "Wala si hivyo viumbe peke yao, bali hata sisi ambao ndio matunda ya kwanza ya Roho, kwa ndani tunalia kwa uchungu tukisubiri kwa shauku kufanywa wana wa Mungu, yaano, ukombozi wa miili yetu" (Warumi 8:23).

Mambo haya yote tunaona leo ni ya muda mfupi siyo ya milele. Tunatazamia wakati ambapo uchungu wa mwili hautakuwa tena. Laana ya Mungu juu ya viumbe siyo laana ya milele. Mungu alipanga kwamba siku moja laana hii itaondolewa kwa viumbe

vyote: “Viumbe vyote vipate kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa kuharibika na kupewa uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu” (Warumi 8:21).

Kristo alikuja katika ulimwengu kukomboa ulimwengu kutoka katika laana hii. Hii ndiyo sababu wakati alikuwa hapa aliwaponya watu wengi. Kulikuwa na wakati ambapo watu walikusanyika kwake na akawaponya wote (Mathayo 8:16; Luka 6:19). Kwa kuwaponya watu alikuwa akionyesha kwamba siku moja ataondoa laana ambayo iko juu ya viumbe. “Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita” (Ufunuo 21:4).

Bwana Yesu alichukua kifo juu yake, na kwa njia hii aliweza kushinda kifo. Wakati alipokuwa msalabani Mungu alimhukumu; kwa hivyo alishinda kifo na magonjwa. Hii ndiyo sababu nabii Isaya anasema, “Alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu iliyotuletea sis amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona” (Isaya 53:5). Bwana Yesu Kristo kwa kifo chake alikomboa viumbe kutokana na laana vilivyokuwamo.

Siku moja kila ugonjwa utaondolewa katika ulimwengu huu. Kutakuwapo na ulimwengu mpya, tutakuwa na miili mipya na hakutakuwa na kifo tena (1 Wakorintho 15:54; 2 Wakorintho 5:4). Biblia inasema, “Mbwa mwitu na mwanakondoo watalisha pamoja, naye simba atakula nyasi kama maksai” (Isaya 65:25). Wale wote ambao wanampenda Kristo wataimba nyimbo za kumshukuru mwana-kondoo ambaye alikufa kwa ajili ya kutukomboa kutoka kwa dhambi, kifo na magonjwa.

# 19.
# Kristo alikufa ili awapatie uzima wa milele wote ambao wanamwamini.

*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).*

Hakuna mwanadamu ambaye anataka kufa. Hata wakati mambo na hali ya maisha ni ngumu sana, huwa tunatazamia wakati ambao mambo yatakuwa mazuri. Kifo ni kitu ambacho huwa hatupendi.

Hii ni kwa sababu kifo ni kitu kibaya sana. Ni adui ambaye anatuondoa katika mambo ya ulimwengu huu, ndiyo mwisho wa tumaini letu la kuishi katika ulimwengu huu. Kila mmoja wetu anataka kuishi na hakuna mmoja ambaye ako tayari kufa.

Hivi ndivyo Mungu ametuumba. "Ameiweka hiyo milele katika ya mioyo ya wanadamu" (Mhubiri 3:11). Tumeumbwa katika mfano wa Mungu na Mungu anapenda maisha na anachukia kifo. Tuliumbwa kuishi milele na tutaishi milele. Kinyume cha maisha ya milele ni jahanum. Mara mingi Yesu alihubiri kuhusu jahanum. "Ye yote anayemwamini Mwana ana uzima wa milele, lakini yeye asiyemwamini Mwana hatauona uzima, bali ghadhabu ya Mungu itakuwa juu yake" (Yohana 3:36).

Bwana Yesu Kristo alifunza wazi kwamba jahanum ni ya milele: "Ndipo hawa watakapoingia kwenye adhabu ya milele, lakini wale wenye haki wataingia katika uzima wa milele" (Mathayo 25:46). Hii ndiyo itatendeka kwa wale wote ambao wanakataa neno la Mungu. Watakuwa katika uchungu wa jahanum milele. Hii ndiyo sababu Yesu alisema, "Nalo jicho lako likikusababisha kutenda dhambi, ling'oe. Ni afadhali kuwa chongo ikaingia katika Ufalme wa Mungu kuliko kuwa na macho mawili na ukatupwa jahanum. Mahali ambako funza wake hawafi, wala moto hauzimiki" (Marko 9:47-48).

Jahanum siyo kama dunia. Hapa duniani kuna matatizo mengi lakini pia kuna vitu vingi vizuri. Mbinguni kuna kila kitu kizuri na jahanum iko na kila kitu kibaya; hakuna anasa au furaha huko.

Wale ambao wameokoka watabadilishwa ili miili yao mipya iweze kufurahia mambo mazuri ya mbinguni: "Lile mambo ambalo jicho halijapata kuona, sikio halijapata kusikia, wala halikuingia moyoni lile Mungu alilowaandalia wale wampendao" (1 Wakorintho 2:9). Hili ni jambo la ukweli kwa wale wote ambao wanamwamini Kristo Yesu. Mbinguni tutaona utukufu wa Mungu. Na uzima wa milele ndio huu, "Wakujue wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma" (Yohana 17:3). Hii ndiyo sababu Kristo aliteseka na akakufa, na ni wale tu ambao watamwamini ndiyo watauona utukufu wa Mungu.

# 20.
# Kristo alikufa ili atuokoe na dunia hii mbovu.

*"Aliyejitoa kwa ajili ya dhambi zetu ili apate kutukoa katika ulimwengu huu mbaya, sawasawa na mapenzi yake Yeye aliye Mungu na Baba yetu" (Wagalatia 1:4).*

Ulimwengu ambao tuishi ndani, katika Biblia unaitwa ulimwengu ambao ni mwovu sana, na mambo itakuwa hivi hadi Bwana Yesu Kristo mwenyewe atakaporudi. Kwa hivyo wakati Biblia inasema kwamba Kristo alijitoa ili atuokoe kutokana ulimwengu huu mwovu, haimaanishi kwamba atatutoa katika ulimwengu huu. Ulimwengu huu utabaki kuwa jinsi ulivyo hadi Kristo atakaporudi. Kile Biblia inamaanisha ni kwamba Bwana Yesu Kristo atatuokoa kutokana na nguvu za mwovu ambazo ziko katika ulimwengu huu. Bwana Yesu Kristo aliomba, "Siombi kwamba uwaondoe ulimwenguni; bali uwalinde na yule mwovu" (Yohana 17:15).

Sababu ya Kristo Yesu kuwaombea watu wake ni, waweze kukombolewa kutoka kwa ulimwengu huu ambao ni mwovu na unatawaliwa na shetani. Shetani hana nguvu zote, lakini ako na nguvu za kudanganya na kuharibu. Biblia inasema kwamba, "Ulimwengu wote uko chini ya utawala wa yule mwovu" (1 Yohana 5:19). Yule mwovu anaitwa mungu wa dunia, na lengo lake kuu ni kuhakikisha kwamba watu hawaelewi neno la Mungu. "Mungu wa dunia hii amepofusha akili za wasioamini, ili wasione nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye sura ya Mungu" (2 Wakorintho 4:4).

Hadi tutakapookolewa, tunaishi maisha kulingana na ulimwengu huu mwovu na tunamtumikia shetani. "Mlizitenda mlipofuatisha namna ya ulimwengu huu na za yule mtawala wa ufalme wa anga, yule roho atendaye kazi ndani ya wale wasiotii" (Waefeso 2:2). Wale wote ambao hawajaokoka ni watumwa wa shetani hata kama hawaelewi jambo hili na kulikataa. Wanafikiria kwamba wao

wako huru, lakini ukweli ni kwamba wao ni watumwa wa shetani. Bibilia inasema hivi kuhusu vitu vya ulimwengu huu, "Huwaahidia uhuru hao waliowanasa, wakati wao wenyewe ni watumwa wa ufisadi. Kwa maana mtu ni mtumwa wa kitu cho chote kinachomtawala" (2 Petro 2:19).

Hii ndiyo sababu Biblia inatuambia kwamba, "Wala msiufuate namna ya dunia hii; bali mgeuzwa kwa kufanywa upya nia zenu" (Warumi 12:2). Kwa ufupi kile Biblia inasema hapa ni kwamba tusifanywe watumwa wa anasa na mali za ulimwengu huu, bali tuwe huru katika Kristo Yesu.

Watu wa ulimwengu huwaza kwamba wao wako huru na ni wenye hekima, lakini Biblia inasema hivi kuwahusu, "Msijidanganye. Kama mtu ye yote miongoni mwenu akidhani kuwa ana hekima kwa viwango vya dunia hii, inampasa awe mjinga ili apate kuwa na hekima. Kwa maana hekima ya ulimwengu huu ni upuzi mbele za Mungu. Kama ilivyoandikwa: 'Mungu huwanasa wenye hekima katika hila yao'" (1 Wakorintho 3:18-19). "Kwa maana ujumbe wa msalaba kwa wale wanaopotea ni upuzi, lakini kwetu sisi tunaokolewa ni nguvu za Mungu" (1 Wakorintho 1:18). Watu wa ulimwengu ambao wanaishi maisha ya dhambi hawako huru, wao ni watumwa wa dhambi. Sisi ambao tumeokoka, "Tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa...nguvu na hekima ya Mungu" (1 Wakorintho 1:23-24).

Wakati Kristo alipokufa msalabani, aliwapa uhuru mamilioni ya watu. Alimshinda shetani na akaziharibu nguvu zake. Hii ndiyo sababu Yesu alisema, "Sasa ni saa ya hukumu kwa ajili ya ulimwengu huu, sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje" (Yohana 12:31). Ujumbe wa Yesu Kristo kwa ulimwengu ni msimfuate shetani ambaye anawafanya watu kuwa watumwa wake, bali mje kwake awape uhuru.

# 21.
# Kristo alikufa ili atupatanishe na Mungu

*"Kwa kuwa kama tulipokuwa adui wa Mungu tulipatanishwa naye kwa njia ya kifo cha Mwanawe, si zaidi sana tukiisha kupatanishwa tutaokolewa kwa uzima Wake" (Warumi 5:10)*

Dhambi imeleta uadui kati ya mwanadamu na Mungu. Wakati Mungu na mwanadamu wanapatanishwa mambo mawili yanatendeka. Kwanza kabisa mawazo ya mwanadamu juu ya Mungu hubadilika kabisa. Mwanadamu ni mwasi dhidi ya Mungu na ni adui wa Mungu hadi wakati anapookolewa. Pili, Mawazo ya Mungu juu ya mwanadamu hubadilika kabisa. Mungu amekasirika kwa sababu ya dhambi za mwanadamu, na hasira hii lazima iondolewe. Njia moja tu ambayo mawazo ya Mungu yanaweza kubadilishwa ni, hadi Mungu mwenyewe ambadilishe mwandamu. Hadi Mungu mwenyewe afanye hivi, mwanadamu ataendelea kuwa adui wa Mungu. Sisi ni waasi wa Mungu na maadui wake, na tutaendelea kuwa maadui hadi Mungu mwenyewe afanye kazi katika mioyo yetu na atubadilishe. Hadi afanye kazi hiyo hatutawahi kubadilika; tutaendelea kuwa maadui wake.

Biblia inatuambia kwamba Mungu hufanya kazi hii ndani mwetu wakati bado tuko maadui. Kwa ufupi Biblia inasema kwamba Mungu hutupatanisha naye wakati sisi ni maadui wake. Biblia inasema hivi kuhusu wale ambao hawajaokoka, "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii" (Warumi 8:7). Hii ndiyo ilikuwa hali ya kila mwanadamu wakati Mungu alimtuma Kristo katika ulimwengu huu atuokoe. Alikufa kwa ajili yetu ili aondoe hasira ya Mungu, na Mungu aweze kupatanishwa na watenda dhambi. Kwa kifo cha Kristo msalabani, aliwaondolea watu wake hatia na akafungua njia ya wateule kushiriki na Mungu. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao" (2 Wakorintho 5:19).

Hii ndiyo sababu wahubiri wa injili wanawaambia watenda dhambi, “Twawaomba sasa ninyi kwa niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu” (2 Wakorintho 5:20). Kile wanamaanisha na haya ni kwamba, “Kuja kwa Yesu na ataondoa dhambi zako na uchafu wako na atakupatanisha na Mungu.”

Biblia inazungumza kuhusu upatanisho kati ya mwanadamu na mwanadamu. Biblia inasema hivi kuhusu hali hii, “Kwa hiyo, kama utaona sadaka yako madhabahuni, ukakumbuka kuwa ndugu yako ana kitu dhidi yako, iache sadaka yako hapo hapo, mbele ya madhabahu, uende kwanza ukapatane na ndugu yako wa kiume au kike, kisha urudi na ukatoe sadaka yako” (Mathayo 5:23-24). Wakati Yesu Kristo anasema kwamba, “Upatane kwanza na ndugu yako,” anamaanisha kwamba tatua ile shida ambayo ndugu yako ako nayo dhidi yako. Kwa njia hiyo hiyo wakati tunapatanishwa na Mungu, dhambi zetu lazima ziondolewe kabisa. Hadi dhambi zetu zitakaposamehewa, hatuwezi kupatanishwa na Mungu.

Biblia inatuambia kwamba wakati Bwana Yesu Kristo alikufa msalabani, aliziondoa dhambi zetu ambazo zilikuwa kinyume na Mungu. Kwa hivyo sasa Mungu hatarajii tulipe chochote kwa ajili ya dhambi zetu au kufanya matendo ambayo tunawaza kwamba yatuletea wokovu. Kristo Yesu amefanya kila kitu ambacho tunahitaji ili tupatanishwe na Mungu. Tunahitaji tu kuja kwa Kristo Yesu kwa imani.

# 22.
# Kristo alikufa ili atulete kwa Mungu

*"Kwa kuwa Kristo naye aliteswa mara moja tu, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, ili awalete ninyi kwa Mungu" (1 Petro 3:18).*

*"Lakini sasa, katika Kristo Yesu ninyi ambao hapo kwanza mlikuwa mbali na Mungu, sasa mmeletwa karibu kwa njia ya damu ya Kristo" (Waefeso 2:13).*

Ujumbe wa ukristo ni injili ambayo ni habari njema. Katika Biblia habari njema ni Mungu mwenyewe na yale ambayo amefanya. Habari njema ni kwamba Mungu ametengeneza njia kwa watu wake waweze kuokolewa na wapatanishwe naye.

Kwa hivyo ujumbe wa ukristo unatuongoza kwa Mungu mwenyewe. Ikiwa tutahubiri ujumbe ambao hatuongozi kwa Mungu, basi hatuhubiri ukweli. Kwa hivyo wokovu ni habari njema kwa sababu tunaongozwa kwa Mungu na kutuletwa katika ushirika na Mungu wa milele. Ujumbe muhimu wa Biblia ni kwamba ndani ya Kristo Yesu, tuna ushirika wa milele na Mungu. Mungu ndiye msingi wa imani ya kikristo na ni yeye ndiye msingi wa wokovu wetu. Ikiwa hatutashiriki na Mungu, basi maisha hayana maana.

Huu ni ukweli ambao tunafaa kuzingatia sana. Kuna watu wengi ambao wanadai kuwa wameokoka na wanazungumza kuhusu msamaha wa dhambi, lakini hawazungumzi mengi kumhusu Mungu na ushirika naye. Wanajua kwamba wao ni watenda dhambi ambao wanamhitaji Mungu au si hivyo waelekee jahanum. Kwa hivyo wanakimbia kwa Kristo Yesu awakomboe kutoka kwa jahanum. Lakini hawaishi maisha matakatifu ambayo yanampendeza Mungu, kwa sababu kwao ushirika na Mungu siyo jambo la maana. Watu kama hawa wanahitaji kuuchunguza wokovu wao vizuri. Mtu ambaye hana haja na ushirika wa kila

siku na Mungu na hajitahidi kuwa mtakatifu, mtu huyo hajaokoka. Sababu ya Kristo kufa ilikuwa atupatanishe na Mungu (1 Petro 3:18).

Sababu ya ujumbe huu kuwa habari njema ni, mwanadamu aliumbwa kuwa katika ushirika na Mungu. Hadi tutakapokuwa na ushirika na Mungu hatutawahi kutosheka na kila wakati tutakuwa tukitafuta furaha. Wakati tumekuja kwa Mungu na kuwa na ushirika naye, ndipo tutakuwa na furaha katika mioyo yetu.

Hili ni jambo ambalo watu wa Agano la Kale walijua vizuri. Daudi alijua njia hii na akasema, "Umenijulisha njia ya uzima; utanijaza furaha katika uwepo wako, pamoja na furaha za milele katika mkono wako wa kuume" (Zaburi 16:11). Mbele za uso wa Mungu kuna furaha tele. Hii ndiyo sababu Kristo alikufa, kutupatanisha na Mungu. Kristo alikuja kuleta furaha na kutosheka kwetu. Hii ndiyo sababu tunafaa kugeuka kutoka katika dhambi za kitambo (Waebrania 11:25) na tuje kwa furaha za milele. Njoo kwa Yesu.

# 23.
# Kristo alikufa ili tuwe mali yake.

*"Vivyo hivyo, ndugu zangu, ninyi mmeifia sheria kwa njia ya mwili wa Kristo, ili mweze kuwa mali ya wengine, Yeye ambaye alifufuka kutoka kwa wafu, ili tupate kuzaa matunda kwa Mungu" (Warumi 7:4)*

*"Je, hamjui ya kwamba miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu akaye ndani yenu, ambaye amepewa na Mungu? Ninyi si mali yenu wenyewe, kwa maana mmenunuliwa kwa gharama. Kwa hivyo, mtukuzeni Mungu katika miili yenu" (1 Wakorintho 6:19-20)*

*"Lichungeni kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe" (Matendo ya Mitume 20:28)*

Swali kuu tunafaa kujiuliza katika maisha yetu ni, mimi ni wa nani? Watu ulimwenguni hawaelewi kwamba wao ni watumwa. Wanawaza kwamba wao wako huru kufanya yale yote ambayo wanataka kufanya kwa sababu wao siyo wa mtu yeyote.

Bwana Yesu Kristo ako na maneno haya kwa watu wote wa ulimwengu huu: "Mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru." Wakati alisema maneno haya, wale ambao alikuwa akizungumzia maneno haya walisema, "Ndipo mtaijua kweli nayo kweli itawaweka huru. Wao wakamjibu, 'Sisi tu wazao wa Abrahamu, nasi hatujawa watumwa wa mtu ye yote. Wawezaje kusema kwamba tutawekwa huru?' Yesu akajibu, 'Amin, amin, nawaambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi." (Yohana 8:32-34).

Biblia ni wazi kwamba hakuna mtu yeyote hapa ulimwenguni ambaye ako huru, sisi sote ni watumwa wa mtu fulani. Watu wengine ni watumwa wa dhambi, wengine ni watumwa wa

Mungu. “Je, hamjui kwamba mnapojitoa kwa mtu ye yote kama watumwa watiifu, ninyi ni watumwa wa yule mnayemtii, aidha watumwa wa dhambi, ambayo matokeo yake ni mauti, au wa utii ambao matokeo yake ni haki...mlipokuwa watumwa wa dhambi, mlikuwa hamtawali na haki...lakini sasa kwa kuwa mmewekwa huru mbali na dhambi na mmekuwa watumwa wa Mungu” (Warumi 6:16, 20, 22).

Wakati Biblia inasema kwamba sisi ni watumwa wa dhambi inamaanisha kwamba hatuko huru kutii sheria ya Mungu na kuifuata. Hadi Mungu mwenyewe atupatie nguvu zake kupitia kwa Roho Mtakatifu ndipo tutaweza kumtii. Hii ndiyo sababu Biblia inasema kwamba, “Lakini Mungu ashukuriwe, kwa kuwa ninyi ambazo kwanza mlikuwa watumwa wa dhambi, mmeuwa watii kutoka moyoni kwa mafundisho mliopewa.” (Warumi 6:17). Wokovu ni kazi ya Mungu. “Mungu atawajalia kutubu na kuijua kweli, ili fahamu zao ziwarudie tena, nao waponyoke katika mtego wa Shetani ambaye amewateka wapate kufanya mapenzi yake” (2 Timotheo 2:25-26).

Ni kifo cha Kristo Yesu ambacho kilinunua watu wake kutoka kwa dhambi. “Ninyi si mali yenu wenyewe, kwa maana mmenunuliwa kwa gharama” (1 Wakorintho 6:19-20). Thamani ambayo alilipa ilikuwa damu yake: “Jilindeni nafsi zenu na mlilinde lile kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi wake. Lichungeni kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe” (Matendo ya Mitume 20:28).

Wakati tunaokolewa, Kristo anatuweka huru. Hii haimaanishi kwamba sasa tunafaa kuishi maisha ya dhambi, bali inamaanisha kwamba sasa tuko huru kumtumikia Mungu. Tunakuwa na uhusiano na Bwana Yesu Kristo: “Vivyo hivyo, ndugu zangu, ninyi mmeifia sheria kwa njia ya mwili wa Kristo, ili mweze kuwa mali ya mwingine, Yeye ambaye alifufuka kutoka kwa wafu, ili kwamba tupate kuzaa matunda kwa Mungu” (Warumi 7:4).

Kristo aliteseka na akakufa ili tuweze kuwa huru kutoka kwa utumwa wa dhambi. Wakati tumeokolewa na kuwa wake, tunaanza kumtii kwa furaha. Wewe huko huru; yaani wewe ni wa Mungu au wa shetani.

# 24.
# Kristo alikufa ili tuweze kuwa na ujasiri wa kuja kwa Mungu.

*"Kwa hiyo, ndugu zangu, kwa kuwa tunao ujasiri wa kupaingia Patakatifu pa Patakatifu kwa damu ya Yesu" (Waebrania 10:19).*

Katika Agano la Kale Waisraeli waliamrishwa kujenga hema ambalo liliitwa Hema la Kukutania. Wakati Waisraeli walitoka Misri na wakafika katika mlima Sinai, Mungu aliwapatia maagizo fulani kuhusu jinsi wanafaa kulijenga hema hilo. Waliambiwa, "Hakikisha kuwa umevitengeneza sawasawa na kile kielelezo ulichoonyeshwa kule mlimani" (Kutoka 25:40).

Baada ya miaka 1,400 Bwana Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni na ilikuwa wazi kwamba hekalu hili lilikuwa mfano wa kile ambacho kilikuwa mbinguni. Katika Agano Jipya tunansoma, "Wanahudumu katika patakatifu palipo mfano na kivuli cha ile iliyoko mbinguni. Hii ndiyo sababu Mose alionywa alipokaribia kujenga hema, akiambiwa: 'Hakikisha kuwa unafanya kila kitu sawasawa na kile kielelezo ulichoonyeshwa kule mlimani" (Waebrania 8:5).

Kwa hivyo hema katika Agano la Kale na makuhani na sadaka yote yalikuwa mfano wa yale yalikuwa mbinguni. Yalikuwa hapo kuwaonyesha watu kwamba ukweli wa mambo haya ulikuwa mkuu zaidi. Katika hema kulikuwepo na mahali ambapo makuhani waliingia kila mara na damu ya wanyama. Kwa njia hiyo hiyo mbinguni kuna mahali ambapo Kristo Yesu aliingia na damu yake. Hakuingia mara kwa mara bali aliingia mara moja.

"Kristo alipokuja akiwa Kuhani Mkuu wa mambo mema ambayo tayari yameshawasili, alipitia kwenye hema iliyokuu zaidi na bora zaidi, ambayo haikujengwa kwa mikono ya binadamu, hii ni kusema, ambayo si sehemu ya uumbaji huu. Hakuingia kwa njia ya damu ya mbuzi na ya ndama, lakini aliingiia Patakatifu pa Patakatifu mara moja tu kwa damu yake mwenyewe, akiisha

kupata ukombozi wa milele" (Waebrania 9:11-12). Hii inamaanisha kwamba wale wote ambao wameokoka wanaweza kuenda kwa Mungu mwenyewe kupitia kwa Kristo Yesu. Katika Agano la Kale ni kuhani mkuu pekee ambaye angeingia katika mahali patakatifu na angeingia mara moja kwa mwaka (Waebrania 9:7). Katika Agano la Kale kulikuwepo na pazia ambalo lilitenga mahali patakatifu. Biblia inatuambia kwamba wakati Kristo Yesu alikufa, "Pazia la hekalu likachanika vipande viwili, kuanzia juu hadi chini" (Mathayo 27:51).

Biblia inatuelezea kwamba hii inamaanisha, "Tunao ujasiri wa kupaingia Patakatifu pa Patakifu kwa damu ya Yesu, kwa njia mpya iliyo haituliyofunguliwa kwa ajili yetu kupitia kwenye lile pazia, yaani, mwili Wake" (Waebrania 10:19-20). Hatuwezi kuingia katika uwepo wa Mungu ikiwa hatujasamehewa dhambi zetu katika Kristo Yesu na kuoshwa kwa damu yake. Tukija katika uwepo wa Mungu ikiwa bado tuko katika dhambi zetu, tutakufa papo hapo. Hakuna chochote ambacho ni kichafu chaweza kuingia katika uwepo wa Mungu. Lakini ikiwa tumeokoka, basi tunaweza kuja katika uwepo wa Mungu bila kutatizika. Damu ya Kristo Yesu imetuosha na tumesamehewa kwa kifo chake.

# 25. Kristo alikufa ili awe kwetu mahali ambapo tunakutana na Mungu

*'Yesu akawajibu, "Libomoeni hili hekalu, nami nitalijenga tena kwa siku tatu!"' (Yohana 2:19-20)*

Bwana Yesu Kristo alikufa ili awe mahali ambapo Mungu anakutana na watu wake. Hii ndiyo sababu Yesu alisema kwamba, "Nitaiharibu hekalu hii na kwa siku tatu nitaifufua." Wakati alisema maneno haya hakuwa anazungumza kuhusu jengo la hekalu la Yerusalemu bali alikuwa anazungumza kuhusu mwili wake.

Yesu Kristo alikuja kuwa mahali ambapo Mungu na watu wake wangekutania. Wakati Bwana Yesu Kristo alikufa msalabani, hekalu na sadaka zilifika kikomo. Mambo haya yote yalipita.

Bwana Yesu Kristo ndiye mahali bora zaidi kuliko hekalu pa kukutana na Mungu. Yesu alisema, "Mkuu kuliko Hekalu yupo hapa" (Mathayo 12:6). Katika Agano la Kale Mungu mwenyewe angekuja katika hekalu lakini si kila wakati. Lakini kuhusu Kristo Yesu Biblia inasema kwamba, "Maana ukamilifu wote wa uungu umo ndani ya Kristo katika umbile la mwili wa kibinadamu" (Wakolosai 2:9). Bwana Yesu Kristo mwenyewe ni Mungu, tunapokutana naye, tunakutana na Mungu.

Katika Agano la Kale kulikuwa na makuhani ambao walikuwa wanadamu wa kawaida, yaani, wenye dhambi kama kila mtu. Biblia inasema hivi kumhusu Bwana Yesu Kristo: "Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani, mwanadamu Kristo Yesu" (1 Timotheo 2:5). Ikiwa unataka kutana na Mungu, kuna njia moja tu: kupitia kwa Kristo Yesu. Hatuhitaji jengo la kanisa au mchungaji au kasisi au mtu yeyote, tunahitaji Kristo Yesu pekee.

Katika Biblia tunasoma wakati mmoja ambao Kristo Yesu alizungumza na mwanamke msamaria. Mwanamke msamaria alimwambia Kristo, "Baba zetu waliambudu kwenye mlima huu, lakini ninyi Wayahudi mnasema ni lazima tukaabudu huko Yerusalemu. Yesu akamjibu, "Mwanamke, niamini, wakati unakuja ambapo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala huko Yerusalemu. Ninyi Wasamaria mnaabudu msichokijua. Sisi Wayahudi tunamwabudu Mungu tunayemjua kwa sababu wokovu unatoka kwa Wayahudi. Lakini saa yaja, tena ipo, ambapo wale waabuduo halisi, watamwabudu Baba katika roho na kweli. Watu wanaoabudu namna hii, ndio Baba anawatafuta" (Yohana 4:20-23).

Hapa Kristo Yesu anafunza kuhusu kuabudu kwa ukweli. Kuabudu kwa kweli hakuhusu ni wapi unaabudia, kwa mlima au kanisani, bali kwa roho na kweli. Katika mji wa Yerusalemu hakuna lile jengo la hekalu leo. Yerusalemu siyo mahali ambapo tunakutana na Mungu. Ikiwa tunataka kumwona Mungu, lazima tuende kwa Kristo Yesu kwa sababu yeye mwenyewe alisema, "Aliyeniona mimi, amemwona Baba" (Yohana 14:9). Ikiwa tunataka kumpokea Mungu lazima tumpokea Kristo kwa sababu alisema, "Anipokeaye mimi, amempokea Yeye aliyenituma" (Mathayo 10:40). Ikiwa tunataka Mungu awe miongoni mwetu wakati tunamwabudu, basi lazima tumtafuta Kristo. Kristo alisema, "Anayemkubali Mwana anaye Baba pia" (1 Yohana 2:23). Ikiwa tunataka kumheshima Baba lazima tumheshimu Kristo. Kristo alisema kwamba, "Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyemtuma" (Yohana 5:23). Wakati Kristo alipokufa na kufufuka alichukua nafasi ya hekalu. Unaweza kuja kwake wakati wowote na mahali popote, siyo tu kanisani.

## 26.
## Kristo alikufa ili ukuhani wa Agano la Kale ukomeshwe na Yeye awe Kuhani wa milele.

*"Basi pamekuwepo na makuhani wengi wa aina hiyo, kwa kuwa kifo kiliwazuia kuendelea na huduma yao ya ukuhani, lakini kwa sababu Yesu aishi milele, anao ukuhani wa kudumu. Kwa hiyo anaweza kuwaokoa kabisa wale wanaomjia Mungu kupitia Kwake, kwa sababu Yeye adumu daima kuomb akwa ajili yao. Kwa kuwa ilitupasa tuwe na Kuhani Mkuu wa namna hii, yaani, aliye mtakatifu, aiye na dosari, aliyetengwa na wenye dhambi na kuinuliwa juu ya mbingu. Yeye alitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zao mara moja tu, alipotoa Mwenyewe" (Waebrania 7:23-27).*

*"Kwa maana Kristo hakuingia kwenye patakatifu palipofanywa kwa mikono ya mwanadamu, ambao ni mfano wa kile kilicho halisi. Yeye aliingia mbinguni penyewe, ili sasa aonekane mbele za Mungu kwa ajili yetu. Wala hakuingia mbinguni ili apate kujitoa Mwenyewe mara kwa mara, kama vile kuhani mkuu aingiavyo Patakatifu pa Patakatifu kila mwaka kwa damu ambayo si yake mwenyewe. Ingekuwa hivyo, ingelimpasa Kristo kuteswa mara nyingi tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Lakini sasa ametokea mara moja tu katika mwisho wa nyakati aiondoe dhambi kwa kujitoa mwenyewe kuwa dhabihu." (Waebrania 9:24-26).*

*"Katika mapenzi hayo sisi tumetakaswa na kufanywa watakatifu kwa njia ya sadaka ya mwili wa Yesu Kristo alioutoa mara moja tu" (Waebrania 10:11-12).*

Katika Biblia tunapata maneno haya: “mara moja.” Maneno haya yanamaanisha kwamba kuna jambo kuu ambalo lilitendeka na halifai kutendeka tena. Ni kama mtu ambaye ananunua shamba, wakati ananunua shamba hilo linakuwa lake na hafai kulinunua tena.

Katika agano la kale kuhani mkuu alikuwa anaingia mahali patakatifu mara moja kila mwaka ili atoe sadaka za wanyama kwa ajili ya dhambi za watu. Sadaka ya kuhani mkuu ilikuwa itolewe mara kwa mara. Mungu alikubali sadaka hizo na aliwasamehe watu dhambi zao lakini mwaka ambao uliyofuata kuhani huyo huyo alihitajika tena atoe sadaka hiyo ndipo watu wasamehewe dhambi zao za mwaka huo.

Sadaka hizi zilikuwa zitolewe kila mwaka kwa sababu hazikuweza kuondoa dhambi kabisa. Biblia inasema kwamba, “Lakini zile dhabihu zilikuwa ukumbusho wa dhambi kila mwaka.” (Waebrania 10:3). Watu walijua kwamba walileta wanyama wakiwa sadaka lakini pia walijua kwamba mambo haya wangeyafanya kila mwaka. Hakuna mnyama ambaye angezifia dhambi za mwandamu. Hata makuhani wenyewe walikuwa kwanza watoe dhabihu ya dhambi zao. Sadaka ya wanyama haingeweze kuleta msamaha wa dhambi wa milele: “Kwa sababu haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi” (Waebrania 10:4).

Watu katika Agano la Kale walijua kwamba siku moja Mungu angeleta sadaka takatifu, ile ambayo ingezibeba dhambi za wanadamu wote na kuziondoa kabisa. Hili ni jambo ambalo walijua kwamba siku moja lingetendeka.

Sadaka hii ni Kristo Yesu mwenyewe. Yeye ndiye sadaka ambayo ilitolewa mara moja. Hakuwa na dhambi ndiyo maana hakutoa dhabihu ya dhambi zake kwanza. Yeye ni wa milele kwa hivyo hahitaji kubadilishwa. Yeye ni mwanadamu kamili ndipo anaweza kuzibeba dhambi za wanadamu na kuzilipia fidia. Kwa hivyo sadaka yake ndiyo sadaka ya mwisho, hatuhitaji mtu mwingine; Kristo peke yake ndiye anayeweza kutusamehe dhambi zetu na kutuosha na atulete kwa Mungu.

# 27.
# Kristo alikufa ili awe kuhani mwenye huruma na mwenye usaidizi

*"Yeye mwenyewe alijaribiwa kwa kila namna, kama vile sisi tujaribiwavyo, lakini Yeye hakutenda dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha rehema kwa uajasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kusaidia wakati wa mahitajii" (Waebrania 4:15-16).*

Wakati Bwana Yesu Kristo alijitoa msalabani kwa ajili yetu, alifanyika kuhani wetu mkuu (Waebrania 9:26). Yeye ndiye anayetuakilisha kwa Mungu. Kifo chake msalabani kilimfurahisha Mungu, kwa hivyo Mungu hatawahi kumkataa wakati anatuakilisha. Kwa hivyo tunapoenda kwa Mungu kupitia kwake Mungu hatatukataa.

Lakini Bwana Yesu Kristo ni zaidi ya sadaka yetu. Aliishi hapa ulimwenguni kwa miaka zaidi ya 30. Wakati huo wote alikumbana na majaribu na mateso kama jinsi sisi tunavyokumbana nayo. Yesu Kristo hakuwahi tenda dhambi lakini alipatana na majaribu ambayo tunapatana nayo. Majaribu ambayo alikutana nayo yalikuwa magumu sana kuliko yale ambayo tunakutana nayo leo kwa sababu shetani alijaribu sana kumfanya Kristo atende dhambi. Yesu Kristo alivumilia hadi mwisho na hakuna wakati alishindwa. Kwa hivyo anajua inamaanisha nini kujaribiwa.

Hii inamaanisha kwamba Bwana Yesu Kristo ana uwezo wa kutuhurumia wakati tunajaribiwa. Aliishi maisha ya kujaribiwa. Alijaribiwa kwa kila hali lakini hakuna wakati alishindwa. Biblia inasema, "Yeye hakutenda dhambi, wala udanganyifu haukuonekana kinywani mwake. Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano, alipoteswa, hakutishia, bali alijikabidhi kwa Yeye ahukumuye kwa haki" (1 Petro 2:22-23).

Kwa hivyo Biblia inasema kwamba anaweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu (Waebrania 4:15). Mwana wa Mungu ambaye amekalia mkono wa kuume wa Mungu anaelewa inamaanisha nini kuhisi uchungu, kushushwa moyo na kujaribiwa kutenda dhambi.

Ukweli huu uko na muhimu mkubwa sana ikizingatiwa zaidi hali yetu. Ukweli huu unamaanisha kwamba tunaweza kuja kwa Kristo kwa maombi kwa sababu Biblia inasema kwamba, "Yeye mwenyewe alijaribiwa kwa kila namna, kama vile sisi tujaribiwavyo, lakini Yeye hakutenda dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha rehema kwa uajasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kusaidia wakati wa mahitaji." (Waebrania 4:15-16).

Mara mingi kuna watu ambao huwaza kwamba wakija kwa Mungu na udhaifu wao, basi Mungu hatawakubali. Wanajua kwamba Mungu ni mtakatifu na wao wenyewe ni wenye dhambi na mbele yake hawana amani. Lakini wanapokumbuka kwamba Bwana Yesu Kristo anajua udhaifu na mateso yao, watapata ujasiri wa kukumbana na majaribu yao. Tunajua kwamba hatatukataa bali anaelewa yale ambayo tunapitia.

# 28.
# Kristo alikufa kutukomboa kutokana na mwenendo wa mababu wetu

*"Kwa maana mnafahamu kwamba mlikombolewa kutoka mwenendo wenu usiofaa ambao mliurithi kutoka kwa baba zenu, si kwa vitu viharibikavyo, yaani, kwa fedha na dhahabu, bali kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ile ya Mwana-kondoo asiye na dosari wala doa" (1 Petro 1:18-19)*

Watu wengi leo wanaamini kwamba mababa zao ambao wamekufa au wanaishi wako na ushawishi katika maisha yao. Wanaamini kwamba hali ya maisha ya mababa zao na dhambi zao zinaendelea kushawishi maisha yao. Wanawaza kwamba maisha yao yako jinsi yalivyo kwa sababu ya dhambi za mababa zao.

Lakini Biblia inasema kwamba, "Mlikombolewa kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu." Biblia inazungumza kuhusu maisha ya wale ambao hawajaokoka, ni maisha matupu ambayo hayana maana na hayana na hayana faida. Maisha haya yanagusia maisha ya mababa zetu kwa sababu tulirithi maisha haya na tabia hizi kutoka kwao. Kifo cha Bwana Yesu Kristo kiliwakomboa watu wake kutoka kwa maisha haya. Hii inamaanisha kwamba wale wote ambao wameokoka hawafai kuwa na wasiwasi kuhusu nguvu na ushawishi wa dhambi za mababa zao.

Kristo anatukomboa kutoka kwa mwenendo ya mababa zetu si kwa vitu viharibikavyo, yaani kwa fedha au dhahabu. Fedha na dhahabu ni vile vitu ambavyo ni vya thamani sana kwa walimwengu. Biblia inasema hapa kwamba vitu hivi haviwezi vikatukomboa kutoka kwa mwenendo wa mababa zetu. Tunajua kwamba hata wale ambao ni matajiri sana ni watumwa wa

tamaduni za mababa zao. Wakati wanaoa au wakati wako na matanga hawako huru kufanya jinsi wanavyotaka, bali wanafungwa kufanya kulingana na tamaduni za mababa zao.

Fedha na dhahabu hazina nguvu za kutukomboa kutoka kwa tamaduni zetu, bali ni damu ya Kristo Yesu ambayo iko na nguvu za kutukomboa kutoka kwa mambo haya yote. Biblia inasema kwamba damu yake ni damu ya thamani, kama ya Mwana-kondoo asiye na ila. Wakati Kristo alikufa kwa ajili ya watu wake, alijua kwamba walikuwa wamefungwa na tamaduni zao. Alikufa ili tuwe huru kutokana na mambo haya. Hii ni moja wapo wa sababu za Kristo Yesu kufa.

Hakuna tamaduni ambazo zinaweza kukufunga wakati umekuja kwa Kristo Yesu kwa imani. Sasa umesamehewa dhambi zako zote, umeoshwa na umevalishwa utakatifu wa Kristo Yesu na kufanywa mwana wa Mungu. “Hakuna uchawi dhidi ya Yakobo, wala hakuna uaguzi dhidi ya Israeli” (Hesabu 23:23). Wakati Yesu Kristo alipokufa alituchukilia baraka zote za mbinguni kwa wale ambao wanamwamini. Mungu akikubariki hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kukulaani.

# 29. Kristo alikufa kutuondoa kwa utumwa wa dhambi

*"Kwake Yeye aliyetupenda na ambaye ametuweka huru kutoka katika dhambi zetu kwa damu Yake, akatufanya sisi kuwa ufalme na makuhani, tumtumikie Mungu Wake ambaye ni Baba yake. Utukufu na uwezo vina Yeye milele na lilele!" (Ufunuo 1:5-6)*

*"Vuvyo hivyo Yesu naye aliteswa nje ya lango la mji ili awatakase watu kwa damu Yake mwenyewe" (Waebrania 13:12)*

Dhambi humwangamiza mwanadamu kwa njia mbili. Kwanza, inatufanya kuwa wenye hatia mbele za Mungu ili tuwe chini ya hukumu wa Mungu. Pili, dhambi hutufanya tuwe wachafu machoni pa Mungu. Dhambi huleta hukumu na dhambi hutufanya watumwa.

Damu ya Kristo Yesu hutuondoa katika mambo haya yote. Kwanza, kwa kifo chake msalabani, Bwana Yesu Kristo alizilipia dhambi zetu na kwa hivyo hatia yetu iliondolewa. Pili, damu ambayo Bwana Yesu Kristo alimwaga inatuosha kutokana na uchafu wa dhambi na kutukomboa kutoka kwa dhambi zetu.

Biblia ni wazi kwamba hadi wakati tutakapotolewa katika utumwa wa dhambi hatuwezi kumtii Mungu. Kristo alisema, "Amri mpya nawapa: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi mpendane" (Yohana 13:34). Hapa Kristo Yesu anatupa mfano wa kufuata, lakini hatuwezi kuufuata hadi tukombolewe kutoka kwa dhambi.

Dhambi ni kitu kibaya ambacho kinahitaji nguvu za Mungu kabla ya kukombolewa. Sisi wenyewe kwa nguvu zetu hatuwezi kujikomboa. Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alikufa; kutukomboa kutoka kwa dhambi.

Jinsi anavyotukomboa ni, kwanza anaondoa hatia ya dhambi kwetu, halafu anatuondoa katika nguvu za dhambi. Mungu kwanza anatusamehe dhambi zetu halafu anatuleta katika ushirika naye, halafu anaanza kufanya kazi ndani mwetu kuondoa dhambi mioyoni mwetu.

Kwa wale ambao wameokoka, nguvu za Mungu zinafanya kazi ndani mwao kuwaondoa kwa maisha ya dhambi. Bado wako na dhambi ndani mwao, lakini Mungu ako anafanya kazi ya kuondoa dhambi hiyo kwa njia ya Roho Mtakatifu. Biblia inazungumza kuhusu tunda la Roho: "Tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi." (Wagalatia 5:22-23). Kwa sababu Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani mwetu, Mungu anasema, "Dhambi haitakuwa na mamlaka juu yenu, kwa sababu hampo chini ya sheria, bali chini ya neema" (Warumi 6:14). Kwa sababu tuko chini ya neema ya Mungu, tuko na nguvu za Mungu ndani mwetu. Hii inamaanishi ya kwamba, pole pole dhambi inaondolewa ndani mwetu na tunageuzwa katika mfano wa Kristo Yesu. Hii ndiyo kazi ya Mungu ambayo anafanya ndani mwetu, ni kwa neema yake. Hii ndiyo sababu Paulo anasema, "Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo na neema yake kwangu haikuwa kitu bure. Bali nilizidi sana kufanya kazi kuliko mitume wote lakini haikuwa mimi, bali ni ile neema ya Mungu iliyokuwa pamoja nami." (1 Wakorintho 15:10). Mungu kwa neema yake anatukomboa kutokana na hatia na utumwa wa dhambi kwa imani ndani ya Kristo.

# 30. Kristo alikufa ili tuweze kufa kwa dhambi na tuishi kwa utakatifu

*"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili juu ya mti, ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi kwa haki" (1 Petro 2:24).*

Biblia inatuambia kwamba Yesu Kristo alikufa msalabani kwa sababu ya watu wake. Wale wameokoka hufa kwa dhambi. Kifo cha Yesu Kristo kilikuwa ni cha kulipia fidia watu wake kwa sababu ya dhambi zao. Hii inamaanisha kwamba hawatahukumiwa milele jahanum. Hii ndiyo sababu Yesu alisema "Nami ninawapa uzima wa milele; hawataangamia kamwe" (Yohana 10:28). Biblia pia inasema "Ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

Biblia pia inatufundisha kwamba wale ambao wameokoka watakufa kwa dhambi kwa sababu Kristo alikufa kwa ajili yao: "Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi" (1 Petro 2:24). Kristo alikufa ili tuwe na maisha ya milele na pia Kristo alikufa ili nasi tufe kwa dhambi. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, "Tumeungana naye katika ufufuo Wake" (Warumi 6:5); "Mmoja alikufa kwa ajili ya wote, kwa hiyo wote walikufa" (2 Wakorintho 5:14).

Wale wamemwamini Yesu Kristo wameungana naye na wamekufa naye. Wakristo wote, "Wamesulibiwa pamoja na Kristo" (Wagalatia 2:20).

Wakati Yesu Kristo alikufa msalabani Kalivari alikufa kwa sababu ya dhambi zetu. Dhambi zetu ziliwekelewa juu yake, na akachukua nafasi yetu na akafa msalabani. Wakati mtu ambaye ameokoka anabatizwa, huwa anaonyesha kwamba amekufa kwa dhambi zake na amefufuka kwa maisha mapya ndani ya Yesu Kristo: "Tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti"

(Warumi 6:4). Ubatizo ni ishara ya kuonyesha ni nini imefanyika ndani ya mtu wakati anaokoka. Maji ni kama kaburi, na yule anayeingizwa ndani ya maji tayari amekufa kwa dhambi zake na ubatizo ni ishara ya hii. “Mkiwa mmezikwa pamoja naye katika ubatizo na kufufuliwa pamoja naye kwa kuuamini uweza wa Mungu aliyemfufua kutoka kwa wafu.” (Wakolosai 2:12).

Mtu ambaye ameokoka amekufa kwa dhambi zake kwa sababu Kristo alimfia; “Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki” (1 Petro 2:24). Hii inamaanisha hatuishi tena jinsi tulivyokuwa tukiishi hapo zamani. Maisha ya dhambi tuliyokuwa tunayaishi kabla hatujaokoka ni lazima yakufe. Tunaanza maisha mapya: yaani tunakufa na kufufuka tena tukiwa tumeokoka.

Tunapookoka basi huwa tunakufa kwa maisha ya kale ya dhambi. Mtu ambaye aliishi maisha ya dhambi na kupenda dhambi ni lazima afe na Kristo Yesu. Mtu huyu dhambi kwake inakuwa si kitu cha kupendeza hata kidogo tena. Anajua kwamba ni dhambi yake ilimfanya Kristo akufe msalabani na ni lazima ayaache maisha yake ya dhambi. Sasa mtu huyu amekufa kwa dhambi na kamwe dhambi haimtawali. Dhambi sasa imekuwa adui wake.

Badala ya kuishi maisha ya dhambi, mkristo huyu anaanza kuishi maisha ya kumpendeza Mungu: “Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki.” (1 Petro 2:24). Dhambi inakuwa si ya kutamaniwa na mioyo yetu, na Kristo anakuwa ndiye wa kutamaniwa na mioyo yetu. Hivi ndivyo Biblia inasema, kwa kila mkristo, “Jitoeni kwa Mungu, kama watu waliotolewa kutoka mautini kuingia uzimani. Nanyi vitoeni viungo vya miili yenu Kwake kama vyombo vya haki.” (Warumi 6:13).

# 31.
# Kristo alikufa ili tukufe kwa Sheria na tuzae matunda kwa Mungu

*"Ninyi mmeifia sheria kwa njia ya mwili wa Kristo, ili mweze kuwa mali ya mwingine, Yeye ambaye alifufuka kutoka kwa wafu, ili kwamba tupate kuzaa matunda kwa Mungu." (Warumi 7:4).*

Wakati Yesu alikufa msalabani, wateule wake waliunganishwa na yeye. Kifo chake kwa sababu ya dhambi zetu kilikuwa kifo chetu ndani yake. Hii inamaanisha tunapookoka tunakufa kwa dhambi na kwa sheria. Sheria ya Mungu inatueleza dhambi ni nini: "Pasipo na sheria, hapana kosa" (Warumi 5:15); "Basi tunajua ya kwamba cho chote sheria inachosema, inawaambia wale walio chini ya sheria ili kila kinywa kinyamazishwe na ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu" (Warumi 3:19).

Sheria huwaletea laana wote wanaoanguka dhambini. Sheria ilitoka kwa Mungu na inatuonyesha makosa yetu mbele ya Mungu. Njia moja tu tunaweza kuwa huru kutoka kwa laana ya sheria ni kulipiwa fidia ya dhambi zetu. Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alikuja: "Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu" (Wagalatia 3:13).

Punde tu tunapookoka sheria ya Mungu haiwezi kutuhukumu kwa sababu Kristo ni mwokozi wetu. Wakati Yesu Kristo aliishi hapa duniani, aliishi maisha matakatifu yasiyokuwa na dhambi na akatimiza mahitaji ya sheria kwa niaba yetu. Wakati alikufa msalabani alilipa fidia kwa niaba yetu.

Hii ndiyo sababu Biblia inasema wazi kwamba wokovu siyo kwa uwezo wetu: "Hakuna binadamu hata mmoja atakayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa matendo ya sheria" (Warumi 3:20); "Mtu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria bali kwa njia ya imani katika Yesu Kristo" (Wagalatia 2:16). Hatuwezi kuokolewa kwa kujaribu kutimiza sheria ya Mungu, bali tumaini letu ni maisha na kifo cha Yesu Kristo: tunaokolewa kwa imani ndani

yake. “Kwa maana twaona kwamba mwanadamu huhesabiwa haki kwa njia ya imani wala si kwa matendo ya sheria” (Warumi 3:28).

Wale ambao wameokoka, maisha yao yanatawaliwa na Kristo wala si sheria. Tunajua kwamba sheria ni nzuri na takatifu (Warumi 7:12), na kama watu wameokoka watatamani kuishi wakifuata sheria ya Mungu. Hatufanyi hivi kwa sababu tunataka tupate wokovu kwa nguvu zetu bali ni kwa sababu tumeokolewa kwa imani. Tunaishi maisha yetu tukiongozwa na Roho Mtakatifu wala si sheria: “Andiko huua, bali Roho hutia uzima” (2 Wakorintho 3:6).

Hii ndiyo sababu Biblia inasema kwamba yule ambaye ameokoka anazaa matunda ya utakatifu: “Ninyi mmeifia sheria kwa njia ya mwili ya Kristo, ili mweze kuwa mali ya mwingine, Yeye ambaye alifiufuka kutoka wafu, ili kwamba tupate kuzaa matunda kwa Mungu.” (Warumi 7:4). Mti huzaa matunda, kwa kawaida huwa haulazimishwi kuyazaa matunda hayo. Ikiwa mti umepata udongo mzuri, basi mti huo utazaa matunda mazuri. Mtu ambaye ameokoka ako na uhusiano mzuri na Yesu Kristo: yeye ni kama mti ambao uko na udongo mzuri na ataishi maisha ya kutii kwa sababu ya uhusiano wake na Yesu.

# 32.
# Kristo alikufa ili atuwezeshe kuishi kwa ajili Yake bali siyo kwa ajili yetu

*“Naye alikufa kwa ajili ya watu wote, ili kwamba wote wanaoishi wasiishi tena kwa ajili ya nafsi Yake Yeye aliyekufa na kufufuka tena kwa ajili yao.” (2 Wakorintho 5:15).*

Msitari huu unaopatikana katika kitabu cha 2 Wakorintho 5:15 unasema kwamba Kristo alikufa ndipo wale ambao wameokoka wamwishie. Yaani, alikufa ili tumtukuze yeye na kumwinua.

Biblia inatueleza wazi kwamba wakati tunaishi maisha ya dhambi huwa tunakosa kumletea Mungu utukufu (Warumi 3:23). Lakini Kristo alikufa ili aondoe dhambi zetu na atukomboe kutoka kwa dhambi ili tusiishi maisha ya dhambi bali tumwishie Kristo. Yesu alikufa ili tuachiliwe kutoka kwa dhambi na tuishi maisha ya kumtukuza.

Kuishi maisha ya kumtukuza Kristo ndilo jambo muhimu sana mtu anaweza kufanya hapa duniani. Bwana Yesu Kristo ni Mungu, na ni mkamilifu katika kila jambo, ni mwenye hekima, ni mwenye haki na huadhibu dhambi. Pia ni Mungu mwenyewe ambaye ako na nguvu zote. “Mwana ni mng’ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake” (Waebrania 1:3). Kwa hivyo jambo mzuri maishani ni kumpenda na kumtumikia Kristo na kuishi tukimtukuza.

Mtume Paulo aliandika: “Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, sasa nayahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara tupu nikiyalinganisha na faida kubwa ipitayo kiasi ya kumjua Kristo Yesu Bwana wangu, ambaye kwa ajili Yake nimepata hasara ya

mambo yote, nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nimpate Kristo" (Wafilipi 3:7-8).

Wakati tunasema ni lazima tumtumikie Kristo, haimaanishi kwamba Kristo hawezi kufanya chochote bila sisi. "Wala hatumikiwi na mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji cho chote" (Matendo ya Mitume 17:25). Si kweli kwamba bila sisi Kristo hawezi kufanya lolote. "Kwa kuwa hata Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai Wake kwa ukombozi kwa ajili ya wengi" (Marko 10:45). Yesu Kristo alikufa ili tuweze kuona utukufu wake. Alikufa ili atutoe kutoka kwa utumwa wa dhambi ili tuwe na furaha ya kumtumikia.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba anaenda mbinguni ili amtume Roho Mtakatifu ambaye ni Msaidizi (Yohana 16:14). Aliwaambia wakati Roho Mtakatifu atakapokuja atamtukuza Yesu Kristo (Yohana 16:14). Kristo alikufa na akafufuka na pia akamtuma Roho Mtakatifu ili tuweze kuona utukufu wake. Hii ndiyo kazi Roho Mtakatifu hufanya, hutuonyesha utukufu wa Yesu Kristo. Hii ndiyo sababu Yesu aliomba, "Baba, shauku Yangu ni kwamba, wale ulionipa wawe pamoja nami pale nilipo, ili waweze kuuona utukufu Wangu, yaani, utukufu ule ulionipa kwa kuwa ulinipenda hata kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu" (Yohana 17:24). Ni kwa sababu hii Kristo alikufa.

# 33.
# Kristo alikufa ili msalaba wake uwe majivuno yetu

*"Mungu apishie mbali nisije nikajivunia kitu cho chote isipokuwa msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa Yeye ulimwengu umesulubiwa kwangu, nami nimesulubiwa kwa ulimwengu" (Wagalatia 6:14).*

Biblia inatuambia kwamba wale wameokoka wanafurahia msalaba kwa sababu ndiyo njia ya wokovu. Inasema tunapaswa "kufurahi katika utukufu wa Mungu" (Warumi 5:2), "katika dhiki pia" (Warumi 5:3), "katika udhaifu" (2 Wakorintho 12:9) na "katika Kristo" (1 Wathesalonike 2:19). Lakini zaidi ya yote tunanapaswa kufurahia katika msalaba wa Yesu.

Sababu ya sisi kufurahia ndani ya msalaba wa Yesu Kristo ni kuwa, huu ndiyo msingi wa imani yetu. Kila kitu kingine hutoka hapa. Tunafurahia wakati wa shida na wakati wa udhaifu wetu kwa sababu ya msalaba. Haingekuwa msalaba wa Yesu hatungefurahia mambo haya.

Biblia inatufundisha kwamba msalaba wa Yesu Kristo hubadilisha kila kitu. Ikiwa mtu hajaokoka atapata hawezi kufurahia msalaba, hawezi akasema kwamba jambo fulani muhimu limemtendekea na kwamba amepata baraka kutoka kwa Mungu. Jambo moja tu atasema ni kwamba yeye ako na shida mingi maishani.

Lakini mtu ambaye ameokoka hufurahia baraka nyingi kutoka kwa Mungu kwa sababu ya kifo cha Yesu Kristo. Hata zile shida anazopata katika dunia hii ni baraka kwake.

Hii inamaanisha kwamba wakristo wanapaswa kukua jinsi wanavyokumbana na mambo. Ikiwa mkristo atakumbwa na matatizo ya maisha, hapaswi kulalamika kama mtu wa dunia bali anapaswa kuwaza kulingana na Biblia kuhusu shida alizo nazo. Anapaswa kuufikiria msalaba wa Kristo na pia anapaswa

akumbuke yeye si mtu wa dunia: “Ulimwengu umesulibishwa kwangu, na nimesulubiwa kwa ulimwengu” (Wagalatia 6:14). Hadi wakati tutafikiria na kutembea katika ukweli wa yale ambayo yalitendeka msalabani, ndipo tunaweza kuishi maisha ya ukristo.

Kwa hivyo wakati mtu ameokoka ulimwengu huwa haumpendezi kamwe. Yeye amekufa kwa mambo ya ulimwengu huu na hayafuati, yeye ni “Kiumbe kipya” (Wagalatia 6:15). Yeye amezaliwa upya katika imani ndani ya Yesu Kristo. Wakati mtu amekuwa kiumbe kipya, anaishi maisha ya kumtumikia Kristo na anaanza kuziacha kabisa anasa za dunia hii. Anajua kwamba anaenda mbinguni kuwa na Yesu Kristo na kwa hivyo anaanza kutilia maanani sana mambo ya Kristo na ufalme wa Mungu.

# 34.
# Kristo alikufa kutuwezesha kuishi kwa imani ndani Yake

*"Nimesulubiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu.." (Wagalatia 2:20).*

Katika msitari huu, Paulo anasema kwamba alisulubiwa na sasa anaishi. Paulo anamaanisha kwamba alikufa na Yesu Kristo na sasa anaishi kwa utukufu wake, yaani Yesu anaishi ndani yake.

Katika msitari huu tunaona maana ya kuokoka. Wakati mtu anaokoka, jambo fulani kubwa hufanyika kwake. Ule utu wake wa kale hufa na badala yake kiumbe kipya hufanyika. "Mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya" (2 Wakorintho 5:17). "Hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema. Mungu alitufufua pamoja na Kristo na kutuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu." (Waefeso 2:5-6).

Wakati Yesu Kristo alikufa aliwachukua watu wake pamoja naye kaburini: walikufa pamoja naye: "Utu wetu wa kale ulisulubiwa opamoja naye ili ule mwili wa dhambi upate kuangamizwa, nasi tusiendelee kuwa tena watumwa wa dhambi." (Warumi 6:6). Wakati tunaokoka tunaunganishwa na Kristo. Utu wa kale hufa.

Katika mstari huu, Paulo anaendelea kueleza hali ya mtu ambaye amezaliwa mara ya pili, yaani mtu ambaye ni kiumbe kipya. Paulo anasema hii kuhusu mtu ambaye ameokoka, "Kristo anaishi ndani mwake." Huu ni ukweli kwa kila mtu ambaye amekoka, kwamba Kristo anaishi ndani yake. Mtu ambaye ameokoka huwa anaishi chini ya mwongozo na utawala wa Yesu Kristo na anaishi maisha yake kwa nguvu za Yesu Kristo. "Naweza kufany amambo yote katik aYeye anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:13); "Ninajitaabisha, nikijitahidi kwa kadiri ya nguvu zile ambazo kwa uwezo mwingi

hutenda kazi ndani yangu" (Wakolosai 1:29). Hii ndiyo sababu mtu ambaye amezaliwa upya husema "Maana sitathubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu" (Warumi 15:18).

Hivi ndivyo msitari wa Wagalatia 2:20 unamaanisha. Kristo anaishi ndani yetu, Kristo anatuongoza na Kristo anatupatia nguvu. Hii ndiyo sababu alikufa ili watu wake waishi kwa imani ndani yake: "Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."

Kwa hivyo kile Paulo anasema hapa ni kwamba mtu akiokoka, Kristo huja na kukaa ndani yake na kutoka wakati huo mtu huyo anaishi maisha ya imani ndani ya Kristo. Kristo anaishi ndani ya watu wake na huwapa mwongozo, uwezo na nguvu. Mtu ambaye ameokoka hupokea haya yote kwa imani.

# 35.
# Kristo alikufa kupatia ndoa maana yake halali

*"Ninyi waume, wapendeni wake zenu, kama vile Kristo alivyopenda Kanisa akajito akwa ajili yake.." (Waefeso 5:25).*

Mungu amepanga ndoa kwamba mume atampenda mkewe kama vile Yesu Kristo anawapenda watu wake. Mke anapaswa kumtii mume kama vile watu wa Yesu wanapaswa kumtii yeye. Yesu alikuwa na sababu hii wakati alikuja kuwaokoa watu wake: alikuja kwa bibi arusi, kumpenda na kufa kwa sababu yake.

Hii haimaniishi kwamba mume anapaswa kufa ili amwokoe bibi yake, bali inamaanisha wanaume wapende wake zao jinsi Kristo alilipenda kanisa kwa njia maalum.

Mambo ya ndoa ni mambo ambayo Mungu alipanga kabla hajaumba Adamu na Hawa. Biblia inatufundisha kwamba wakati Mungu alianzisha ndoa, alikuwa anapanga kuhusu Kristo na kanisa wala si Adamu na Hawa. Hii ndiyo sababu Paulo anasema, "Kwa sababu hii, mwanamume atamwacha baba yake na mama yake, naye ataambatana na mkewe na hawa wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hii ni kubwa, bali mimi nanena kuhusu Kristo na Kanisa." (Waefeso 5:31-32).

Hii inamaanisha kutoka mwanzo Mungu alipanga ndoa ili aonyeshe uhusiano wa Kristo na kanisa lake. Uhusiano huu huonekana wazi wakati Kristo alikuja na kufa kwa sababu ya kanisa. Kwa hivyo tunapotazama ndoa kati ya mwanamume na mwanamke, tunaona uhusiano wa Kristo Yesu na kanisa lake.

Wakati Kristo alikufa msalabani Kalivari, alikuwa anawaza kuhusu watu wake. Yesu alijua wakati alikuwa anaenda msalabani kufa kwamba kifo chake kitawaonyesha watu wake maana ya kweli ya ndoa. Wakati aliteseka, alikuwa anawafundisha wanaume jinsi ya kuwapenda wake zao.

Tukiangalia duniani leo tunaona kwamba ndoa nyingi hazina raha. Hivi sivyo Mungu alikusudia, hili ni jambo ambalo lililetwa na dhambi. Dhambi imo mioyoni mwetu na hii ndiyo sababu wanaume hawapendi wake zao jinsi wanafaa kuwapenda. Pia kwa sababu hii wake hawawatii jinsi wanapaswa kutii waume zao. Yesu aliteseka na kufa ili aondoe dhambi hii. Na kwa sababu ya kifo chake Kristo Yesu, hatufai sasa kusema kwamba hata nisipompenda mke wangu au kumtii mume wangu jinsi ninafaa kumpenda ni kwa sababu ya dhambi. Kristo alikufa ili atuonyesha jinsi ya kuisha na wake na waume wetu. (Waefeso 5:22-25).

# 36.
# Kristo alikufa kukomboa watu ambao wako na hamu ya kufanya kazi ya Mungu

*"Alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe miliki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema" (Tito 2:14).*

Ujumbe wa Biblia ni kwamba tumesamehewa makosa yetu yote na kwamba kumekubalika mbele za Mungu siyo kwa sababu tumefanya kazi mzuri lakini ni kwa imani ndani ya Kristo. Mungu anatuokoa bila malipo ndiyo tuweze kufanya mambo mazuri. Biblia inasema, "Ambaye alituokoa na kutuita katika mwito mtakatifu, si kwa matendo yetu mema" (2 Timotheo 1:9). Kwa hivyo kazi mzuri hazituokoi, tunafanya kazi mzuri baada ya kuokoka. Kazi mzuri ni matunda ya wokovu na siyo mizizi ya wokovu. Yesu Kristo alikufa, "Kujisafishia watu kuwa mali Yake Mwenyewe, yaani, wale walio na bidii katika kutenda mema." (Tito 2:14).

Biblia inaeleza wazi kwamba wokovu ni kwa imani, siyo kitu ambacho tunapata kwa sababu tumefanya kazi. Ni zawadi tunapewa bila malipo kutoka kwa Mungu. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:8-9). Yesu aliteseka na kufa ili kazi mzuri iwe ndiyo matunda ya imani ya ukristo wetu baada ya kuokolewa kwa imani.

Hii ndiyo sababu Biblia inasema, "Tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili tupate kutenda matendo mema" (Waefeso 2:10). Hii inamaanisha tumeokolewa kwa imani ili tutende matendo mema baada ya kuokoka. Hii haimaanishi kwamba matendo mazuri ndiyo yanatuokoa, lakini matendo mazuri yanakuja baada ya

kuokoka. Bwana Yesu Kristo hatupatii tu uwezo wa kutenda matendo mazuri, bali anatupatia bidii ya kufanya matendo mazuri. Hii ndiyo sababu Biblia inasema kwamba watu wa Mungu wanapaswa kuwa na juhudi ya kutenda matendo mema. Kuwa na juhudi juu ya jambo inamaanisha kutia bidii sana katika jambo hilo. Yesu alikufa ili tuwe na juhudi sana ya kufanya matendo mema. Yesu Kristo hataki tuwe na mioyo nusu nusu kuhusu matendo mazuri. Wale wameokoka wanapaswa kutia juhudi ya kuwa watakatifu kwa mioyo yao yote.

Sababu kuu kwa nini Yesu Kristo anataka tufanye matendo mema ni ili tuweze kumletea utukufu Mungu. Yesu alisema, “Nuru yenu iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.” (Mathayo 5:16). Wakati tunatenda matendo mema huwa tunamletea utukufu Mungu. Ni kwa sababu hii Kristo alikufa msalabani.

Wakati watu wa Mungu wanatenda matendo mazuri humu duniani, dunia huwa inayaona. Watu wa dunia ni watu wachoyo, hawafanyii wenzao matendo mazuri bali wanajifikiria tu wenyewe. Wakati wakristo wanawashughulikia wengine na kuwafanyia matendo mazuri Mungu huwa anatukuzwa.

Wakati Biblia inaongea kuhusu matendo mema, inamaanisha kuwasaidia wale wako na shida na mahitaji. Kwa mfano Biblia inasema, “Watu wetu hawana budi kujifunza kujitoa kutenda mema, ili waweze kuwasaidia watu wenye mahitaji ya lazima ya kila siku, wasije wakaishi maisha yasiyokuwa na matunda.” (Tito 3:14). Hii ndiyo sababu Kristo alikufa, ajisafishie watu wake wenye juhudi ya kutenda matendo mazuri, hasa hasa kuwasaidia maskini na wale wote ambao wako na mahitaji.

# 37.
# Kristo alikufa kutuita tufuate mfano wake wa upole na upendo wenye gharama kubwa sana.

*"Kwa maana ni jambo la sifa kama mtu akivumilia anapoteswa kwa uonevu kwa ajili ya kumkumbuka Mungu. Kwa kuwa ninyi mliitwa kwa ajili ya hayo, kwa ajili yenu, akiwaachia kielelezo, ili mzifuaye nyayo zako." (1 Petro 2:19:21).*

*"Mtafakarini sana Yeye aliyestahimili upinzani mkuu namna hii kutoka kwa watu wenye dhambi, ili kwamba msije mkachoka na kukata tamaa. Katika kushindana kwenu dhidi ya dhambi, bado hamjapigana kiasi cha kumwaga damu yenu" (Waebrania 12:3-4)*

*"Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu. Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya si kitu, akajifanya sawa na mtumwa, akazaliwa katika umbo la mwanadamu,. Naye akiwa na umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba!" (Wafilipi 2:5-8)*

Tunapookoka, tunaanza kuufuata mfano wa Yesu Kristo. Yesu Kristo ni mwokozi wetu na pia ni mfano wetu. Akiwa mwokozi, anatuokoa kutoka kwa dhambi zetu, na akiwa mfano kwetu hutufundisha jinsi ya kuishi maisha ya kumpendeza Mungu.

Biblia inafundisha wazi kwamba kabla hatujaanza kuufuata mfano wa Kristo ni lazima kwanza tuokolewe naye. Mtu ambaye hajaokoka hawezi akaishi kama Kristo kwa sababu yeye ni mtumwa wa dhambi.

Tunapookolewa kupitia kwa imani ndani ya Yesu Kristo tunakuwa watu wapya. Biblia inasema tunakuwa viumbe vipya. Tunakombolewa kutoka kwa dhambi zetu na tunapewa uwezo wa kutii na kufuata Kristo. Tunapaswa kwanza kumwamini Yesu Kristo kuwa mwokozi kabla hatujaanza kuufuata mfano wake.

Mtume Paulo alisema anatamani kuwa na haki ya Kristo kwa imani na kushiriki katika mateso pamoja na Kristo katika kazi yake. "Nami nionekane mbele Zake nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu kwa njia ya imani. Nataka nimjue Kristo na uweza wa kufufuka Kwake na ushirika ya mateso Yake, ili nifanane naye katika mauti Yake." (Wafilipi 3:9-10). Mpangilio huu uko wazi: kwamba unaokolewa kwanza halafu tunafuata mfano wa Kristo.

Biblia inatuamru "Ninavumilia mambo yote kwa ajili ya wateule wa Mungu, kusudi wao nao wapate wokovu ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele" (2 Timotheo 2:10). Hii inamaanisha tunapovumilia matatizo na shida za maisha, tunawaelekeza watu kwa Kristo. Jinsi tunavyovumilia shida kwa uvumilivi tunaonyesha ulimwengu jinsi tunaye mwokozi mkuu.

# 38.
# Kristo alikufa kuumba jamii moja ya wafuasi ambao wanajitolea kwake.

*"Ye yote anayetaka kunifuata ni lazima ajikane mwenyewe, achukue msalaba wake kila siku na anifuate" (Luka 9:23).*

*"Ye yote asiyeuchukua msalaba wake na kunifuata, hastahili kuwa Wangu" (Mathayo 10:38).*

Yesu Kristo alikufa ili awe na wafuasi ambao wataacha yote ya dunia kwa sababu yake. Biblia inatuambia kwamba Yesu Kristo alikuwa tayari kwenda Kalivari na, "Alikaza uso Wake kwenda Yerusalemu" (Luka 9:51). Hakuna mmoja angeweza kumzuia kwenda Kalivari na kutoa maisha yake kuwa sadaka kwa watu wake, Yeye mwenyewe aliamua kufanya hivyo. Wakati mtu mmoja alimwambia akiwa njiani kwenda Yerusalemu kwamba atakuwa hatarini kwa sababu ya Herode, Yesu alisema, "Nendeni mkamwambia yule mbweha, 'Ninafukuza pepo wachafu na kuponya wagonjwa leo na kesho, nami siku ya tatu nitaikamilisha kazi Yangu" (Luka 13:32). Yesu aliendа Yerusalemu akijua kwamba atashikwa na kuhukumiwa kifo. Wakati umati wa watu ulimshika, usiku huo kabla hajakufa alisema "Haya yote yametukia ili maandiko ya manabii yapate kutimia" (Mathayo 26:56).

Yesu aliteseka na anatarajia wafuasi wake wawe tayari kufuata njia hiyo hiyo. Yesu aliamua kufuata njia ya Kalivari ambayo ilikuwa na mateso mengi, na pia anataka wafuasi wake wafanye jinsi alivyofanya. Yesu anasema, "Ye yote anayetaka kunifuata ni lazima ajikane mwenyewe, achukue msalaba wake kila siku na anifuate" (Luka 9:23). Wakati Yesu Kristo alienda msalabani, nia yake kuu ilikuwa kuumba jamii moja ya wafuasi ambao wanajitolea kwake.

Yesu anatuambia tuubeba msalaba wetu kila siku. Hii inamaanisha kwamba ikiwa tutaokolewa ni lazima tufe kwa dhambi zetu, kama vile Yesu Kristo alikufa kwa sababu ya dhambi zetu. Wakati Yesu Kristo anamwambia mtu ambaye ameokoka aubeba msalaba wake kila siku, huwa anamwambia aache dhambi zake na aishi maisha matakatifu. Ikiwa hatutaishi maisha matakatifu na badala yake kuishi kama watu wa dunia, basi sisi hatutakuwa wafuasi wa Yesu Kristo. Yesu alisema, “Ye yote asiyeuchukua msalaba wake na kunifuata, hastahili kuwa Wangu.” (Mathayo 10:38).

Hii inamaanisha kwamba wakati mtu anadai kwamba ameokoka, anapaswa kuendelea kuziacha dhambi zake na kufuata mfano wa Kristo kila wakati. Yeye ni lazima aangamize dhambi zake zote na awe kama Kristo. “Vivyo hivyo, jihesabuni wafu katika dhambi lakini mlio hai kwa Mungu, kama watu watu waliotolewa kutoka mautini kuingia uzimani. Nanyi vitoeni viungo vya miili yenu Kwake kama viombo vya haki.” (Warumi 6:11).

Kuubeba msalaba ni zaidi ya kupigana na dhambi. Inamaanisha ni lazima tuwe tayari kupata aibu kwa sababu ya Yesu Kristo. “Vivyo hivyo Yesu naye aliteswa nje ya lango la mji ili awatakase watu kwa damu Yake mwenyewe. Kwa hiyo basi na tumwendee nje ya kambi, tukiichukua aibu aliyobeba” (Waebrania 13:12-13). Watu watatucheka sana wakati tunaokoka na hata katika nchi zingine watu wanauawa kwa sababu ya imani yao. Biblia inasema kuhusu watu hao ambao wanauliwa: “Nao wakamshinda kwa damu ya Mwanakondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa” (Ufunuo 12:11). Kwa hivyo Mwana-kondoo alimwaga damu yake ili tumshide shetani kwa kuamini katika damu yake na tufe katika dhambi zetu. Haya ndiyo maisha Kristo anatuitia.

# 39. Kristo alikufa kutukomboa kutoka kwa uoga wa kifo

*"Basi kwa kuwa watoto wana nyama na damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao na kuwaweka huru wale waliokuwa utumwani maisha yao yote kwa sababu ya kuogopa mauti" (Waebrania 2:14-15)*

Yesu alimwita shetani mwuuaji: "Yeye alikuwa mwuuaji tangu mwanzo; wala hakushikana na kweli maana hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo uongo" (Yohana 8:44). Haja kuu ya shetani si kuua mtu bali ni kuhakisha mtu huyo ataishi milele jahanum. Shetani anataka wafuasi wake wafurahiye maisha ya anasa za dhambi hapa duniani na mwishowe kuhukumiwa milele jahanum. Hii ndiyo shetani anataka kwa wafuasi wake.

Tunahitaji kukumbuka kwamba si shetani anawapeleka watu jahanum bali ni dhambi zao ndiyo zinazowapeleka watu hawa jahanum. Jambo moja tu ambalo litamfanya mtu kwenda jahanum ni kwa sababu ya kukosa kutubu dhambi zake na kumwomba Bwana Yesu msamaha. Shetani hawezi kutuma mtu jahanum, anaweza tu kuwadanganya watu. Shetani huwadanganya watu kwamba maisha ya dhambi ni mazuri na hakuna haja ya kuokoka. Ikiwa watu wanakataa kudanganywa, shetani hana mamlaka kabisa.

Hii ndiyo kazi Kristo alikuja kufanya, kuondoa uwezo wa shetani wa kuwadanganya watu. Ili afanye hivi, Kristo alizichukua dhambi zetu na akazikufia msalabani. Baada ya kuchukua dhambi zetu na kuzilipia fidia msalabani, shetani hana uwezo tena wa kuwazuia watu wa Mungu kuokoka. Sasa shetani hana uwezo wowote wa kuwaangamiza wale wameokoka. Ghadhabu ya Mungu imeondolewa, na huruma ya Mungu ikawa ndiyo ngao yetu na shetani hawezi akafaulu dhidi yetu.

Kwa sababu Yesu Kristo alikuwa anakuja kutuokoa sisi, ilimbidi awe mwanadamu kamili ili apitie mauti. Ni kifo cha Mwana wa Mungu pekee kingeondoa nguvu za shetani. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, “Basi kwa kuwa watoto wana nyama na damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao” (Waebrania 2:14). Yesu alikuwa mwanadamu kamili kwa sababu watu wale alikuja kuwaokoa walikuwa wanadamu kamili. Wakati Kristo alikufa alizichukua dhambi zetu, kwa hivyo shetani hana uwezo wa kutuhukumu.

Kwa hivyo kusudi la Yesu lilikuwa hili: uoga wa kifo uondolewe. Kupitia kifo chake, “na kuwaweka huru wale waliokuwa utumwani maisha yao yote kwa sababu ya kuogopa mauti” (Waebrania 2:15). Uoga kwa sababu ya kifo hutufanya kuwa watumwa kwa sababu hatujui ni nini itafanyika baada ya kufa. Lakini kifo cha Yesu huondoa uoga huo wote. Wale wote wameokoka wamehakikishiwa nafasi mbinguni na hawapaswi kuogopa kamwe.

Mauti inaweza tu kuua miili yetu wala haiui nafsi. Nafsi zetu ziko kwa Kristo. Na wakati Yesu Kristo atakaporudi, miili yetu itafufuliwa tena: “Nanyi ikiwa Roho wa Mungu aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu anakaa ndani yenu, Yeye aliyemfufua Kristo Yesu kutoka kwa wafu ataihuisha pia miili yenu ambayo hufa kwa njia ya Roho Wake akaaye ndani yenu” (Warumi 8:11). Wale wameokoka wamewekwa huru kutoka kwa kila uoga, na Biblia inatueleza jinsi ya kutumia huru wetu: “Ndugu zangu, ninyi mliitwa ili mwe huru, hivyo msitumie uhuru wenu kama fursa ya kufuata tamaa za mwili, bali tumikianeni ninyi kwa ninyi kwa upendo.” (Wagalatia 5:13).

# 40.
# Kristo alikufa ili tuweze kuwa naye baada ya kufa kwetu

*"Yeye alikufa kwa ajili yetu ili kwamba kama tuko macho au tukiwa tumelala tupate kuishi pamoja Naye." (1 Wathesalonike 5:10)*

*"Kwa maana kwangu mimi, kuishi ni Kristo na kufa ni faida; Ninavutwa kati ya mambo mawili: Ninatamani kuondoka nikae pamoja na Krsito, jambo hilo ni bora zaidi." (Wafilipi 1:21,23)*

*"Naam, tunalo tumaini na ingekuwa bora zaidi kuuacha mwili huu na kwenda kukaa na Bwana." (2 Wakorintho 5:8)*

Biblia haisemmi kwamba miili yetu ni mibaya. Kuna dini zingine ambazo zinaamini kwamba mwili ni mbaya na nafsi yetu ndiyo tu safi. Lakini imani ya ukristo haifundishi hivyo. Kwetu wakristo, kifo ni adui kwa sababu kinaua miili yetu. Hivi ndivyo Biblia inasema kuhusu miili yetu: "Mwili wa mwanadamu haukuumbwa kwa ajili ya zinaa bali kwa ajili ya Bwana na Bwana kwa ajili ya mwili." (1 Wakorintho 6:13). Bwana ni kwa mwili, kumaanisha Mungu anashughulika na miili yetu.

Lakini wakati tunakufa, mwili na nafsi hutengana. Mwili unazikwa kwa mchanga na kuoza. Na nafsi inaenda kukaa na Bwana. Hii ni faraja kubwa kwa wale wameokoka, kwa sababu nafsi zitakuwa na Bwana.

Biblia inasema mwili ni kama nguo kwa nafsi: "Kwa sababu hatutaki kuvuliwa bali kuvikwa makao yetu ya mbinguni ili kwamba kile kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima." (2 Wakorintho 5:4). Kile Paulo anasema hapa ni kwamba angependa kutoka kwa huu mwili wa duniani na kuingia katika mwili wa ufufuo. Hakuwa anataka wakati ambapo nafsi iwe bila mwili.

Wale ambao wako hai watageuzwa na kupewa miili mipya wakati Kristo atakaporudi.

Paulo tena anaongea kuhusu wakati nafsi itakuwa na Bwana bila mwili. Anasema, “Kuishi ni Kristo, na kufa ni faida” (Wafilipi 1:21). Nafsi kuwa na Yesu Kristo ni faida kubwa hata ikiwa haina mwili. Hii ni kwa sababu mtu ameokoka akifa anaenda kuwa na Yesu. Hii ndiyo maana Paulo anasema, “Ninatamani kuondoka nikae na pamoja na Kristo, jambo hilo ni bora zaidi.” (Wafilipi 1:23).

Kuwa na Kristo, Paulo anasema ni vizuri zaidi kuliko kuwa katika mwili hapa duniani. Ni vizuri zaidi kwa sababu nafsi yake iko na Kristo na imetoka katika ulimwengu wa dhambi na maumivu. Hii ndiyo sababu Paulo anasema, “Naam, tunalo tumaini na ingekuwa bora zaidi kuuacha mwili huu na kuenda kuwa na Bwana” (2 Wakorintho 5:8). Wale wameokoka wataenda kukaa na Bwana wakikufa na wataishi naye kwa amani na furaha. Watakuwa nyumbani naye.

Hii ni mojawapo ya sababu kuu kwa nini Kristo alikufa. “Yeye alikufa kwa ajili yetu ili kwamba kama tuko macho au tukiwa tumelala tupate kuishi pamoja Naye.” (1 Wathesalonike 5:10). Mwili utaenda mchangani, bali nafsi itakuwa na Bwana mbinguni. Na wakati Bwana atakaporudi, atampatia kila mtu mwili mpya ambao utaishi milele.

# 41.
# Kristo alikufa kuhakikisha kufufuka kwetu kutokak wa wafu.

*“Kwa maana ikiwa tumeungana naye katika mauti Yake, bila shaka tutaungana naye katika ufufuo Wake” (Warumi 6:5)*

*“Nanyi ikiwa Roho wa Mungu aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu anakaa ndani yenu, Yeye aliyemfufua Kristo Yesu kutoka kwa wafu ataihuisha pia miili yenu ambayo hufa kwa njia ya Roho Wake akaaye ndani yenu.” (Warumi 8:11)*

*“Hili ni neno la kuaminiwa: Kwa maana kama tumekufa pamoja naye, tutaoishi pamoja naye.” (2 Timotheo 2:11)*

Bwana Yesu alifanya miujiza mingi wakati alipokuwa hapa ulimwenguni. Alimfufua mtoto msichana wa miaka 12 na wanaume wawili ambao walikuwa wamekufa (Marko 5:41-42; Luka 7:14-15; Yohana 11:43-44). Lakini wale watu ambao aliwafufua hawakuishi milele katika miili hiyo kwani walikufa tena. Wakati Bwana Yesu Kristo alipofufuka kutoka kwa wafu, alishinda nguvu za kifo ili watu wote ambao wamepewa miili ya ufufuo wasije wakakufa tena.

Wakati Mungu alipomfufua Bwana Yesu Kristo kutoka kwa wafu, Mungu alikuwa anasema kwamba Bwana Yesu Kristo alifaulu katika kutulipia fidia ya dhambi zetu. Sadaka ambayo alitoa msalabani ilikubalika na Mungu. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, “Alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba! Kwa hiyo, Mungu alimtukuza sana na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina.” (Wafilipi 2:8-9). Wakati Kristo alipokuwa msalabani alilia kwa sauti akisema, “imekwisha” (Yohana 19:30). Wakati Mungu alipomfufua Kristo kutoka kwa wafu, Mungu alikuwa akisema, “Kweli imekwisha!” Kristo alikuwa amefidia dhambi zetu msalabani na alituondoa katika nguvu za dhambi.

Siku tatu baada ya kifo chake, Kristo alishinda kifo. Kwa sababu alifufuka, kifo hakina nguvu tena za kuwaangamiza miili ya ufufuo wa watu wote. Hii ndiyo sababu Kristo anasema, “Mimi ni Alpha na Omega”, asema Bwana Mungu, “Aliyeko, aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi” (Ufunuo 1:8).

Biblia ni wazi kwamba wale wote ambao wameokoka watafufuliwa kutoka kwa wafu naye Kristo na watakaa naye milele. “Kwa maana ikiwa tumeungana naye katika mauti Yake, bila shaka tutaungana naye katika ufufuo Wake.” (Warumi 6:5). “Kwa kuwa tumeamini kwamba Yesu alikufa na kufufuka, hata hivyo, Mungu kwa njia ya Yesu atawafufua pamoja naye wale waliolala mautini.” (1 Wathesalonike 4:14). “Naye Mungu aliyemfufua Bwana kutoka kwa wafu atatufufua sisi pia kwa uweza Wake.” (1 Wakorintho 6:14).

Biblia inatufundisha jinsi Bwana Yesu alivyoshinda nguvu za kifo. Biblia inasema, “Uchungu wa mauti ni dhambi na nguvu ya dhambi ni sheria.” (1 Wakorintho 15:56). Hii inamaanisha kwamba sisi sote tumetenda dhambi na tutahukumiwa milele. Biblia inaendelea kusema, “Lakini ashukuriwe Mungu, Yeye atupaye ushindi kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.” (1 Wakorintho 15:57). Kwa ufupi hitaji la torati lililipwa kwa maisha na kifo cha Bwana Yesu Kristo. Wakati dhambi zetu zinasamehewa, torati haiwezi kutuhukumu kwani haina nguvu ya kutugusa, hatuwezi kuhukumiwa milele. Badala yake, “Ghafla, kufumba na kufumbua, parapanda ya mwisho itakapolia. Kwa kuwa parapanda italia, nao wafu watafufuliwa na miili isiyoharibika, nasi tutabadilishwa. Kwa hiyo, mwili huu wa kuharibika utakapovaa kutoharibika, nao huu mwili wa kufa utakapovaa kutokufa, ndipo lile neno lililoandikwa litakapotimia: ‘ Mauti imemezwa kwa kushinda’ ” (1 Wakorintho 15:52;54). Hii ndiyo sababu Yesu anakuita uje kwake. “Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi” (Yohana 11:25).

# 42. Kristo alikufa kuzivua enzi na mamlaka.

*"Akiisha kuifuta ile hati yenye mashtaka yaliyokuwa yanatukabili pamoja na amri zake, aliiondoa isiwepo tena, akiigongomea kwenye msalaba Wake. Mungu akiisha kuzivunja enzi na mamlaka, alizifanya kuwa kitu cha fedheha hadharani kwa kuziburuza kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba wa Kristo." (Wakolosai 2:14-15)*

*"Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi za Ibilisi." (1 Yohana 3:8)*

Kuna wakati katika Biblia ambapo mistari kama huu wa enzi na mamlaka humaanisha serikali za ulimwengu huu. Lakini tunaposoma kwamba msalabani Kristo alizivua enzi na mamlaka na kuzifanya mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo, Biblia inazungumza kuhusu nguvu za shetani ambazo hutawala ulimwenguni. Tunaona jambo hili wazi katika Waefeso 6:12 wakati Biblia inasema kwamba, "Kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo katika ulimwenguni wa roho."

Katika Biblia shetani anaitwa "mungu wa dunia" mara tatu. Wakati Kristo alikuwa karibu kufa msalabani, alisema, "Sasa ni saa ya hukumu kwa ajili ya ulimwengu huu, sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje." (Yohana 12:31). Kwa kifo cha Bwana Yesu Kristo shetani alishindwa na mapepo wake. Wote walishindwa msalabani.

Jambo hili halimaanishi kwamba wao hawako tena ulimwenguni. Hata sasa tunapigana nao. Lakini tunapigana na maadui ambaye ameshaa shindwa. Sisi tunajua kwamba tuko na ushindi. Ni kama mnyama ambaye kichwa chake kimekatwa na anakimbiakimbia

hapa na pale akiwa na ukali mwingi hadi wakati atakapoanguka afe. Vita vimesha shindwa, lakini tunafaa tuwe waangalifu sana kwa sababu shetani bado anaweza kuleta uharibifu.

Wakati Bwana Yesu Kristo alikufa, Mungu alikuwa, "Akiisha kuifuta ile hati yenye mashtaka yaliyokuwa yanatukabili pamoja na amri zake, aliiondoa isiwepo tena, akiigongomea kwenye msalaba Wake." (Wakolosai 2:14). Hivi ndivyo alivyozivua enzi na mamlaka na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri. Kwa ufupi sheria ya Mungu haituhukumu tena kwa sababu Kristo alilipa fidia ya dhambi zetu. Shetani hawezi tena kutushitaki.

Kabla ya Kristo Yesu kuzifidia dhambi zetu, shetani alikuwa akiwashitaki watu wake. Jina shetani linamaanisha adui au mwenye kutushitaki. Lakini baada ya kifo cha Bwana Yesu Kristo, jambo muhimu lilitendeka. "Kisha nikasikia sauti kuu mbinguni ikisema, 'Sasa Wokovu na weza na Ufalme wa Mungu wetu umekuja na mamlaka ya Kristo wake. Kwa kuwa ametupa chini mshtaki wa ndugu zetu, anayewashtaki mbele za Mungu usiku na mchana." (Ufunuo 12:10). Kristo amemshinda mshitaki na amemtupa chini.

Sasa baada ya kuokoka hakuna mashitaka yanaweza kuletwa dhidi yetu. "Ni nani atakayewashtaki wale ambao Mungu amewachagua? Ni Mungu mwenyewe ndiye mwenye kuwahesabia haki." (Warumi 8:33). Hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kuwashitaki wateule wa Mungu. Kristo ndiye haki yetu kwa hivyo mshitaki wetu amevuliwa mamlaka. Hawezi kutushitaki tena, na akifanya hivi ataibishwa. Kwa hivyo watu wa Mungu wako huru kumtumikia Mungu kwa furaha. Hatumtumikii Mungu tukiwa katika utumwa au uoga, tunamtumikia kwa sababu tumewekwa huru ili tuweze kumtumikia.

# 43.
# Kristo alikufa ili aachilie nguvu za Mungu katika injili

*"Kwa maana ujumbe wa msalaba kwa wale wanaopotea ni upuzi, lakini kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu" (1 Wakorintho 1:18)*

*"Mimi siionei haya Injili ya Kristo kwa maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwanza kwa Myahudi na kwa Myunani pia" (Warumi 1:16)*

Neno "injili" linamaanisha habari njema. Wakati tunapohubiri injili tunatangaza habari ambazo zinawaletea watu furaha kwa sababu ni habari njema. Injili ni habari njema kwa sababu kweli itawafanya watu wawe na furaha ya milele.

Ujumbe wa injili ni kifo na kufufuka kwa Bwana Yesu Kristo. Mtume Paulo anasema jambo hili wazi wakati anasema, "Basi ndugu zangu nataka niwakumbushe kuhusu Injili niliyowahubiria, mkaipokea na ambayo katika hiyo mmesimama. Kwa Injili hii mnayookolewa mkishikilia kwa uthabiti neno nililowahubiria ninyi. La sivyo, mmeamini katika ubatili. Kwa maana yale niliyopokea ndiyo niliyowapa ninyi, kama yenye umuhimu wa kwanza: Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yasemayo Maandiko, ya kuwa alizikwa na alifufuka siku ya tatu, na kwamba alimtokea Kefa, kisha akawatokea wale kumi na wawili. Baadaye akawatokea wale ndugu waamini zaidi ya 500 kwa pamoja, ambao wengi wao bado wako hai, ingawa wengi wamelala. Ndipo akamtokea Yakobo na kisha mitume wote." (1 Wakorintho 15:1-7).

Ujumbe wa injili ni huu: Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, alizikwa, alifufuliwa na aliwatokea zaidi ya watu mia tano. Kwa hivyo ujumbe wa injili unahusu mambo ambayo yalitokea. Ujumbe huu hauhusu mawazo ya watu au hisia za watu, unahusu

mambo ya ukweli ambayo yalitokea: kuzikwa na kufufuliwa kwa Kristo Yesu.

Kwa watu wengi ulimwenguni, ujumbe wa injili ni upumbavu kwao. Biblia inasema kwamba, “Kwa maana ujumbe wa msalaba kwa wale wanaopotea ni upuzi, lakini kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu” (1 Wakorintho 1:18). Hizi ndizo nguvu ambazo Kristo wakati alikufa aliachilia katika injili.

“Mimi siionei haya Injili ya Kristo kwa maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwanza kwa Myahudi na kwa Myunani pia.” (Warumi 1:16).

Ni kwa nini kifo cha Bwana Yesu Kristo ni habari njema kwa wengi na ni upuzi kwa wengine? Kwa nini watu wengine hawamwamini Kristo ili waokolewe? Jibu la maswali haya limepeanwa katika Biblia: “Kwa habari yao, mungu wa dunia hii amepofusha akili za wasioamini, ili wasione nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye sura ya Mungu.” (2 Wakorintho 4:4). Kuongezea kwa haya ni kwamba mwanadamu amekufa katika dhambi zake na hawezi kuelewa ukweli ambao unatoka kwa Mungu. “Mtu ambaye hana Roho wa Mungu hawezi kupokea mambo yatokayo kwa Roho wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa sababu hayo yanaeleweka tu kwa jinsi ya rohoni.” (1 Wakorintho 2:14).

Kabla ya mtu yeyote kuokolewa, macho yake lazima yafunguliwe na apewe uhai wa kiroho. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, “Lakini kwa wale ambao Mungu amewaita, yaani, Wayahudi na Wayunani, Kristo ni nguvu na hekima ya Mungu” (1 Wakorintho 1:24). Sisi sote wakati moja tulikuwa tumepofushwa na shetani na tulikuwa tumekufa katika dhambi zetu. Lakini Mungu aliondoa upofu wetu na akatufanya kuwa hai kiroho. Hivi ndivyo tulivyookolewa. Ikiwa hujaokoka, basi wewe umepofushwa na shetani na umekufa katika dhambi zako. Mwombe Mungu akuondolee upofu wako na akufanye kuwa hai katika Kristo.

# 44.
# Kristo alikufa kuharibu uadui kati ya makabila za ulimwengu.

*"Kwa maana Yeye mwenyewe ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi tuliokuwa wawili, yaani, Wayahudi na watu wa Mataifa tuwe wamoja kwa kuvunja kizuizi na kubomoa ule ukuta wa uadui uliokuwa kati yetu. Kwa kuibatilisha ile sheria pamoja na amri zake na maagizo yake alipoutoa mwili wake, ili apate kufanya ndani yake mtu mmoja mpya badala ya hao wawili, hivyo, akifanya amani" (Waefeso 2:14-16).*

Katika Agano Jipya tunasoma kuwahusu Wayahudi na watu wa Mataifa. Ni wazi kwamba kulikuwepo uadui kati ya watu hawa. Mfano wa haya ni katika kitabu cha Wagalatia 2:11-12, "Lakini Petro alipofika Antiokia, mimi nilimpiga ana kwa ana kwa sababu alikuwa amekosa kwa wazi. Kabla baadhi ya watu waliotoka kwa Yakobo hawajafika, alikuwa akila pamoja na watu wa Mataifa. Lakini hao watu walipofika alianza kujiondoa na kujitenga na watu Mataifa kwa sababu aliwaogopa wale wa kundi la tohara."

Kefa (yaani Petro) alikuwa akiishi katika uhuru wa Kristo hata kama alikuwa Myahudi. Alikuwa akila na watu wa mataifa kwa sababu kwake hakukuwa na uadui kati yake na watu wa mataifa ambao walikuwa wameokoka. Lakini wakati Wayahudi ambao walishikilia desturi sana walikuja Antiokia, Kefa aliwaogopa sana. Kwa hivyo aliacha kula na watu wa mataifa na akawa sasa anakula tu na Wayahudi pekee. Aliogopa kwamba wale Wayahudi ambao walikuwa wamekuja Antiokia wangemkemea sana.

Wakati Paulo aliona yale ambayo yalikuwa yametendeka, alikasirika kwa sababu ya tabia ya Kefa. Siyo jambo jema machoni pa Mungu mkristo kukataa kushiriki na mkristo mwingine kwa sababu ya kabila. Wakati Paulo aliona ni nini inatendeka, aliongea na Kefa uso kwa uso kumrekebisha kuhusu

mambo haya (Wagalatia 2:14). Wale wote ambao wako na ukabila wanakataa ujumbe wa injili. Wakati Kefa alikataa kushiriki na wakristo wa mataifa alikuwa anakataa ujumbe wa injili. Kristo alikufa kwa ajili ya watu wake wote na kwa hivyo hatufai kuwa na ukabila miongoni mwetu.

Kwa hivyo wakati Paulo aliona kile ambacho kilikuwa kikifanywa na Kefa, alizungumza mbele ya watu kwamba, "Wewe ni Myahudi, nawe unaishi kama mtu wa Mataifa na wala si kama Myahudi. Imekuwaje basi, mnawalazimisha watu Mataifa kufuata desturi za Kiyahudi?" (Wagalatia 2:14). Wakati Kefa alikataa ushirika na watu wa mataifa alikuwa akisema, lazima muwe Wayahudi ndipo niweze kushiriki nanyi. Ni kama mtu leo aseme, lazima uwe mtu wa kabila yangu ndipo uwe mshirika wa kanisa langu. Lakini Bwana Yesu Kristo aliondoa mambo haya yote wakati alipokufa msalabani.

Kristo alikufa ili makabila ya ulimwengu yapatanishwa kwake. Anawaleta pamoja watu wake wote, haijalishi wanatoka katika kabila gani au rangi gani au nchi gani, wote ni wake.

Utenganisho ambao uko katika ulimwengu kote ni kati ya wale ambao wameokoka na wale ambao hawajaokoka. Wale wote ambao wameokoka ni wa Mungu na ni watoto wake wapendwa. Wale wote ambao hawajaokoka ni wa shetani. Watu hawa hawako katika ufalme wa Mungu na hawataingia mbinguni wakati watakapokufa. Kristo Yesu ndiye njia ya pekee mtu yeyote anaweza kuingia ufalme wa Mungu.

# 45.
# Kristo alikufa kuwa fidia ya watu kutoka kila kabila, rangi na taifa

*“Wewe unastahili kukitwaa kitabu na kuzivunja lakiri zake, kwa sababu ulichinjwa na kwa damu Yako ukamnunulia Mungu watu kutoka katika kila kabila, kila lugha, kila jamaa na taifa “ (Ufunuo 5:9)*

Katika mstari huu tunatazama kile ambacho kinatendeka mbinguni. Mtume Yohana alikubaliwa kuona kile ambacho kitakuwa kikitendeka huku mbinguni milele. “Kisha nikaona katika mkono Wake wa kuume yule aliyeketi kwenye kiti cha enzi, kitabu kilichoandikwa ndani na upande wa nyuma kikiwa kimefungwa kwa lakiri saba.” (Ufunuo 5:1). Muhuri ni hesabu ya kila kitu ambacho kitatendeka hapa ulimwenguni. Moja wa malaika alimwambia Yohana, “Simba wa kabila la Yuda, wa uzao wa Daudi, ameshinda, ili kwamba aweze kukifungua hicho kitabu na kuvunja hizo lakiri zake saba” (Ufunuo 5:5). Simba wa kabila la Yuda ni Kristo Yesu. Ameshinda kifo, kwa kifo chake na kufufuka kwake. Yohana alimwona, “Mwana-Kondoo amesimama, akiwa kama amechinjwa” (Ufunuo 5:6).

Malaika wote waliaanguka chini na kuanza kumwabudu. Waliimba wimbo mpya wakisema kwamba kwa sababu Kristo Yesu alikufa, ako na uwezo wa kufungua muhuri wa kihistoria. Kile malaika hawa wanamaanisha ni kwamba, kwa sababu ya kifo cha Bwana Yesu Kristo, sasa Yeye ndiye Bwana wa kihistoria: Yeye anadhibiti kila kitu ambacho kinatendeka hapa ulimwenguni. Nao waimba wimbo mpya wakisema, “Wewe unastahili kukitwaa kitabu na kuzivunja lakiri zake, kwa sababu ulichinjwa na kwa damu Yako ukamnunulia Mungu watu kutoka katika kila kabila, kila lugha, kila jamaa na taifa” (Ufunuo 5:9).

Kristo alikufa kuwaokoa watu wa aina tofauti kutoka kila taifa la ulimwenguni. Watu wa ulimwengu wametenda dhambi. Kila taifa ulimwenguni linahitaji wokovu. Hii ndiyo sababu Yesu Kristo

alikuja ulimwenguni: alikuja kuwaokoa watu kutoka kila taifa la ulimwengu. Ugonjwa wa dhambi uko kila mahali na tabibu pia wa ugonjwa huu ako kila mahali. Kristo Yesu alisema, “Lakini Mimi, nikiinuliwa kutoka katika nchi, nitawavuta watu wote waje Kwangu.” (Yohana 12:32). Msalabani Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya watu kutoka kila taifa la ulimwengu.

Ukristo ulianza katika nchi ya Uisraeli na baadaye ukaenea bara Uropa. Sasa imeenea katika kila pembe la ulimwengu. Katika Agano la kale tunaambiwa kwamba hili jambo lilikuwa litendeke: “Miisho yote ya dunia watasherehekea na kuabudu, wote waendao mavumbini watapiga magoti mbele yake, wote ambao hawawezi kudumisha uhai wao.” (Zaburi 22:27). “Mataifa yote wafurahi na kuimba kwa shangwe, kwa kuwa unatawala watu kwa haki na kuongoza mataifa ya dunia” (Zaburi 67:4). Kwa hivyo wakati huduma wa Kristo Yesu ulifika kilele hapa ulimwenguni, alitangaza mpango wake wazi wazi: “Haya ndiyo yaliyoandikwa: Kristo atateswa na siku ya tatu atafufuka kutoka kwa wafu. Toba na msamaha wa dhambi utatangazwa kupitia Jina Lake, kuanzia Yerusalemu” (Luka 24:46-47). “Kwa sababu hii, enedeni ulimwengu mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi” (Mathayo 28:19).

Bwana Yesu Kristo siyo mwokozi tu wa mataifa fulani au makabila fulani. Yeye si wa taifa moja pekee. “Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!” (Yohana 1:29). “Kwa maana hakuna tofauti kati ya tofauti kati ya Myahudi na Myunani, Yeye ni Bwana wa wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao. Kwa maana, ‘Kila mtu atakayeliita Jina la Bwana, ataokoka’ ” (Warumi 10:12-13). Mwite sasa na ungane na watu wake ambao wako katika kila pembe la ulimwengu.

# 46.
# Kristo alikufa kukusanya kondoo wake kutoka kwa kila pembe la ulimwengu.

*"Hakusema haya kutokana na mawazo yake mwenyewe bali kama Kuhani Mkuu mwaka huo, alitabiri kuwa Yesu angalikufa kwa ajili ya Wayahudi, wala si kwa ajili ya Wayahudi peke yao, bali pia kwa ajili ya watoto wa Mungu waliotawanyika, ili kuwaleta pamoja na kuwafanya wawe pamoja" (Yohana 11:51-52)*

*"Ninao kondoo wengine ambao si wa zizi hili, inanipasa kuwaleta, nao wataisikia sauti yangu, hivyo patakuwa na kundi moja na mchungaji mmoja" (Yohana 10:16)*

Wakati moja punda alitamka neno la Mungu (Hesabu 22:28). Wakati mwingine mhubiri au kuhani pia anaweza kutamka neno la Mungu bila kujua kile anasema. Jambo hili lilifanyika kwa mtu ambaye aliitwa Kayafa na alikuwa kuhani mkuu wakati wa Kristo. Wakati Kristo alikuwa mbele ya baraza la Wayahudi, Kayafa alisema, "Ni afadhali mtu mmoja afe kwa ajili ya watu" (Yohana 11:50). Kayafa alikuwa akisema kwamba ni vyema Kristo afe badala ya taifa zima liangamizwe na Warumi. Lakini Biblia inasema kwamba, "Hakusema haya kutokana na mawazo yake mwenyewe bali kama Kuhani Mkuu mwaka huo, alitabiri kuwa Yesu angalikufa kwa ajili ya Wayahudi, wala si kwa ajili ya Wayahudi peke yao, bali pia kwa ajili ya watoto wa Mungu waliotawanyika, ili kuwaleta pamoja na kuwafanya wawe pamoja" (Yohana 11:51-52).

Kristo mwenyewe alisema, "Ninao kondoo wengine ambao si wa zizi hili, inanipasa kuwaleta, nao wataisikia sauti yangu, hivyo patakuwa na kundi moja na mchungaji mmoja" (Yohana 10:16).

Mistari hii yote inafunza kitu kimoja. Inamaanisha kwamba ulimwenguni kote kuna watu ambao Mungu amechagua na wataokolewa na Kristo Yesu. Hao ni watoto wa Mungu waliotawanyika, na hao ndiyo Kristo anamaanisha wakati anasema kondoo wengine ninao ambao si wa zizi hili: yaani siyo Wayahudi. Mungu anakujikusanyia watu kutoka kila taifa la ulimwengu. Anawaita watumishi wake waende katika ulimwengu wawafanya watu kuwa wanafunzi wake na pia anaenda nao. Ako na watu ambao alichagua kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu. Yesu alisema kwamba, "Wale wote anipao Baba watakuja Kwangu na ye yote ajaye Kwangu, sitamfukuza nje kamwe. Nimewajulisha Jina Lako wale ulionipa kutoka katika ulimwengu" (Yohana 6:37; 17:6).

Kwa hivyo Biblia inatufunza kwamba Mungu ako na watu wake kwa kila taifa la ulimwengu, na kwamba anawatuma watu wake kwa kila taifa la ulimwengu kuhubiri injili ili watu wake waokoke. Hakuna njia nyingine wanaweza kuokoka: watu wake lazima wahubiri injili. "Mlinzi humfungulia lango na kondoo huisikia sauti yake. huwaita kondoo wake kwa majina yao na kuwatoa nje ya zizi. Akiisha kuwatoa nje, hutangulia mbele yao na kondoo humfuata kwa kuwa wanaijua sauti yake" (Yohana 10:3-4).

Kristo aliteseka na akafa ili kondoo wake waweze kusikia sauti yake na waishi. Hiki ndicho kile Kayafa alisema, hata kama hakujua ni nini alikuwa akisema: Kristo alikuwa afe si kwa ajili ya Wayahudi pekee, lakini pia kuwakusanya watoto wa Mungu ambao walikuwa wametawanyika ulimwenguni kote. Alikufa ili awalete kondoo wake kwa Mungu na awaokoe milele.

# 47.
# Kristo alikufa ili atuondoe katika hukumu wa mwisho.

*"Vivyo hivyo Kristo alitolewa mara moja tu kuwa dhabihu ili azichukue dhambi za watu wengi, naye atakuja mara ya pili, si ili kuchukua dhambi, bali kuwaletea wokovu wale wanaomngoja kwa shauku" (Waebrania 9:28)*

Wakati Biblia inazungumza kuhusu wokovu, inazungumza kuhusu wokovu ambao tayari tumepewa, wokovu ambao tunapewa, na wokovu ambao tutapewa. Biblia inasema, "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani" (Waefeso 2:8). Pia inasema kwamba injili ndiyo "Lakini kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu" (1 Wakorintho 1:18). Inaendelea kusema kwamba, "Sasa wokovu wetu umekaribia zaidi kuliko hapo kwanza tulipoamini" (Warumi 13:11). Kwa ufupi Biblia inafunza kwamba tumeokolewa, tunaokolewa na tutaokolewa.

Katika wokovu huu tunaokolewa na kifo cha Bwana Yesu Kristo. Tumeokolewa kwa sababu Bwana Yesu Kristo alitulipia fidia ya dhambi zetu na akatusamehe. Tunaokolewa kutoka kwa dhambi ambazo bado ziko mioyoni mwetu. Dhambi hizi zinaondolewa na Roho Mtakatifu ambaye Kristo alituma baada ya kupaa mbinguni. Siku ya hukumu tutaokolewa kwa sababu Kristo Yesu alikufa kwa ajili yetu na anatulinda kutokana na hukumu na hasira ya Mungu.

Kuna hukumu ambayo inakuja. Biblia inasema, "Lakini kinachobaki ni kungoja kwa hofu hukumu ya moto uwakao utakaowaangamiza adui za Mungu" (Waebrania 10:27). Biblia inatusihi "Tumwabudu Mungu kwa namna inavyompendeza, kwa unyenyekevu na uchaji, kwa kuwa 'Mungu wetu ni moto ulao'" (Waebrania 12:28-29).

Yohana mbatizaji aliwaonya watu wa siku zake kuhusu hasira itakayokuja (Mathayo 3:7). Siku ya hukumu, "na kuwapa ninyi

mnaoteseka raha pamoja na sisi, wakati Bwana Yesu atakapodhihirishwa kutoka mbinguni katika mwali wa moto pamoja na malaika wake wenye nguvu. Atawaadhibu wale wasiomjua Mungu na ambao hawakutii Injili ya Bwana wetu Yesu. Wataadhibiwa kwa uangamivu wa milele na kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa uweza Wake." (2 Wathesalonike 1:7-9).

Biblia ni wazi kwamba adhabu ya watenda dhambi kule jahanum ni kali sana na ni ya kutisha. Yule ambaye hajaokoka, "Atakunywa mvinyo wa hasira kali ya Mungu ambayo imemiminwa katika kikombe cha ghadhabu yake pasipo kuchanganywa na maji. Naye atateswa kwa moto uwakao na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele za Mwana-Kondoo" (Ufunuo 14:10-11).

Tunapojua jinsi adhabu ilivyo kali, basi tunajua ukuu wa wokovu wetu na, "Kumngojea Mwanawe kutoka mbinguni, ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, yaani, Yesu, Yeye aliyetuokoa kutoka katika ghadhabu inayokuja" (1 Wathesalonike 1:10). Ni Bwana Yesu Kristo pekee ambaye anaweza kutuokoa kutokana na hasira ya Mungu ambayo inakuja. Bila Yeye tutaangamia.

Wale ambao wameokoka wanajua kwamba wakati Kristo atakaporudi watakuwa salama kwa sababu wameokolewa kwa damu yake. "Vivyo hivyo Kristo alitolewa mara moja tu kuwa dhabihu ili azichukue dhambi za watu wengi, naye atakuja mara ya pili, si ili kuchukua dhambi, bali kuwaletea wokovu wale wanaomngoja kwa shauku" (Waebrania 9:28). Kristo ameangamiza dhambi mara moja na alishinda. Hatuhitaji sadaka nyingine yoyote. Ngao yetu dhidi ya hasira ya Mungu na hukumu wa Mungu ni Kristo Yesu. Aliteseka na akafa kwa niaba yetu.

# 48.
# Kristo alikufa kupata furaha yake na yetu

"Tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu" (Waebrania 12:2)

Barabara ambayo inatuongoza katika furaha ya milele mbinguni ni ngumu sana. Ni barabara ngumu sana kwetu na pia ilikuwa barabara ngumu kwa Kristo kwa sababu ilimgharimu maisha yake. Kwa furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba. Kwanza kabisa kulikuwa na uchungu wa msalaba, halafu baadaye furaha ya mbinguni. Hakukuwa njia nyingine.

Kuna sababu mingi kwa nini Bwana Yesu Kristo alikuwa na furaha kubwa sana baada ya kifo chake msalabani. Kwanza, alikuwa na furaha ya kuungana na Babake: "Utanijazia furaha katika uwepo wako, pamoja na furaha za milele katika mkono wako wa kuume" (Zaburi 16:11). Pili, alikuwa na furaha kwa sababu alishinda nguvu za dhambi: "Akiisha kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko mbinguni" (Waebrania 1:3). Tatu, alikuwa na furaha kwa sababu alikalishwa mkono wa kuume wa Mungu Baba: "Naye ameketi kwa mkono wa kuume wa Mungu" (Waebrania 12:2). Nne, alikuwa na furaha kwa sababu watu ambao alikufia wanamzingira wakimsifu: ""Kutakuwa na furaha zaidi mbinguni kwa sababu ya mwenye dhambi mmoja atubuye" (Luka 15:7).

Kwa hivyo Bwana Yesu Kristo alikuwa na furaha kubwa sana wakati alipokufa msalabani. Bibilia inasema kwamba sisi ambao tumeokoka tunashiriki naye katika furaha hii. "Nimewaambia mambo haya ili furaha Yangu iwe ndani yenu na furaha yenu iwe kamili" (Yohana 15:11). Alijua kwamba angekuwa na furaha kubwa ndiyo maana alisema, "Furaha yangu iwe ndani yenu." Sisi ambao tumemwamini tutafurahia kwa furaha kubwa.

Barabara ya furaha ya milele ni ngumu sana. Yesu alisema, "Ulimwenguni mnayo dhiki" (Yohana 16:33). "Mwanafunzi hawezi kumzidi mwalimu wake wala mtumishi hamzidi bwana wake. Yatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake na mtumishi kuwa kama bwana wake. Ikiwa mkuu wa nyumba ameitwa Beelzebuli, je, si zaidi sana wale wa nyumbani mwake mwenyewe!" (Mathayo 10:24-25). "Baadhi yenu watauawa. Mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya Jina langu" (Luka 21:16-17). Bwana Yesu Kristo hakuwaahidi wanafunzi wake maisha yenye starehe hapa ulimwenguni. Aliwaambia wazi kwamba watakumbana na mateso mengi. Hii ndiyo barabara ya kuelekea katika uzima wa milele.

Tunajua kwamba Bwana Yesu Kristo alivumilia msalaba kwa sababu alijua kwamba kulikuwa na furaha kubwa mbele yake. Kwa njia hiyo hiyo sisi pia tunaweza kuvumilia mateso katika maisha haya kwa sababu baada ya maisha haya kutakuwepo na furaha tele. Yesu alisema, "Ni heri ninyi watu watakapowashutumu na kuwatesa na kunena dhidi yenu mabaya ya aina zote kwa uongo kwa ajili yangu. Furahini na kushangilia kwa maana thawabu yenu ni kuu" (Mathayo 5:11-12). Siku moja hata sisi tutakuwa na furaha mbele ya Mungu.

Kwa sababu Yesu Kristo alikufa msalabani kwa ajili yetu, jinsi tutavyotazama mateso yetu inafaa iwe tofauti sana. Sisi siyo kama watu wa ulimwengu ambao hawezi kuvumilia mateso na majaribu. Tunavumilia mateso kwa sababu ya kile ambacho kiko mbele yetu. "Nayahesabu mateso yetu ya wakati huu kuwa si kitu kulinganisha na utukufu utakaodhihirishwa kwetu" (Warumi 8:18). Hii ndiyo sababu mtu ambaye ameokoka anatazama mateso na majaribu kwa njia tofauti kabisa. Anajua kwamba kuna furaha ya milele ambayo inamngojea. "Inawezekana kilio kikawepo usiku kucha, lakini asubuhi kukawa na furaha" (Zaburi 30:5).

# 49.
# Kristo alikufa ili aweze kuvikwa taji la utukufu na heshima

*“Amevikwa taji ya utukufu na heshima kwa sababu alistahimili mauti, ili kwamba kwa neema ya Mungu apate kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu” (Waebrania 2:9)*

*“Bali alijifanya si kitu, akajifanya sawa na mtumwa, akazaliwa katika umbo la mwanadamu. Alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba! Kwa hiyo, Mungu alimtukuza sana na kumpa jina lililo kuu kuliko kila jina” (Wafilipi 2:7-9)*

*“Anastahili Mwana-Kondoo, Yeye aliyechinjwa, kupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na sifa” (Ufunuo 5:12)*

Usiku kabla ya Kristo kufa msalabani Kalivari, aliomba, “Baba, unitukuze mbele Zako kwa ule utukufu niliokuwa nao pamoja na Wewe kabla ulimwengu haujakuwako” (Yohana 17:5). Aliomba kwa Babaye ili aweze kupewa utukufu. Babake alijibu maombi yake: “Amevikwa taji ya utukufu na heshima kwa sababu alistahimili mauti, ili kwamba kwa neema ya Mungu apate kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu” (Waebrania 2:9). Kwa sababu alijitolea kufa kwa ajili ya watu wake, Mungu Baba amemvika na taji la utukufu. “Alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba! Kwa hiyo, Mungu alimtukuza sana na kumpa jina lililo kuu kuliko kila jina” (Wafilipi 2:8-9). “Anastahili Mwana-Kondoo, Yeye aliyechinjwa, kupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na sifa!” (Ufunuo 5:12). Kristo Yesu alipokea utukufu kutoka kwa Mungu Baba kwa sababu alitii Baba hata kwa mauti.

Biblia inatufunza kwamba sababu ya Yesu Kristo kuvikwa na utukufu na heshima, ni aweze kuwaletea watu wake furaha na

kutosheka. Fikiria juu ya mwanamume mmoja na mke wake ambao wamealikwa kwa sherehe fulani. Lakini wakati wanafika huko mwanamume anapokelewa kwa heshima kubwa sana na kutukuzwa machoni pa kila mtu. Je, mke wake atajihisi aje? Kwa kawaida atajihisi mwenye furaha sana kwa sababu mume wake anaheshimiwa na kutukuzwa na watu wote. Kwa njia hiyo hiyo, kanisa la Bwana Yesu Kristo ndiyo bibi arausi wake. Wakati Bwana Yesu Kristo anavikwa heshima na Mungu Baba, watu wa Mungu wanakuwa na furaha mingi sana; kwa sababu mtu ambaye wanampenda amevikwa na heshima na utukufu na Mungu Baba. Kwa hivyo utukufu wa Kristo Yesu unawaletea watu wake furaha kubwa.

Hii ndiyo sababu usiku kabla afe, Bwana Yesu Kristo aliomba, “Baba, shauku Yangu ni kwamba, wale ulionipa wawe pamoja nami pale nilipo, ili waweze kuuona utukufu Wangu, yaani, utukufu ule ulionipa kwa kuwa ulinipenda hata kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu” (Yohana 17:24). Bwana Yesu Kristo anataka tuuone utukufu wake ili tupate furaha.

# 50.
# Kristo alikufa kuonyesha kwamba uovu mbaya sana umekusudiwa na Mungu kwa manufaa ya watu wake

*"ni kweli Herode na Pontio Pilato pamoja na watu Mataifa na waisraeli, walikusanyika katika mji huu dhidi ya Mwanao Yesu uliyemtia mafuta. Wao wakafanya yale ambao uweza wako na mapenzi yako yalikuwa yamekusudia yatokee tangu zamani" (Matendo ya Mitume 4:27-28).*

Tunaishi katika ulimwengu ambao umejaa magonjwa na matatizo. Lakini Biblia inatufunza kwamba watu wa Mungu, wale ambao wameokoka, Mungu anahakikisha kwamba majaribu na mateso yetu yanatuletea manufaa kwa nafsi zetu. Hatuwezi kabisa kuelewa jambo hili, lakini Biblia inasema, "Mambo ya siri ni ya BWANA Mungu wetu." (Kumbukumbu la Torati 29:29).

Mara mingi katika Biblia tunasoma jinsi Mungu anavyobadilisha mambo mabaya kuwa mazuri. Katika kitabu cha Mwanzo, Yusufu aliuzwa katika nchi ya Misri na mandugu zake. Kwa miaka mingi Yusufu aliteseka katika nchi ya Misri. Lakini mwishowe, aliona kwamba huu ulikuwa mpango wa Mungu na kwamba Mungu alimtumia katika nchi hiyo kuwaokoa watu wa Israeli. Aliwaambia mandugu zake kwamba, "Mlikusudia kunidhuru, lakini Mungu alikusudia mema ili litimie hili linalofanyika sasa, kuokoa maisha ya watu wengi" (Mwanzo 50:20).

Kwa njia hiyo hiyo, wakati Waisraeli walitaka mfalme, walitenda dhambi dhidi ya Mungu. Walimwambia Samweli, "Tunataka mfalme wa kututawala" (1 Samweli 8:19). Na baadaye walisema, "Tumeongezea uovu juu ya dhambi zetu nyingine kwa kuomba mfalme" (1 Samweli 12:19). Lakini Mungu alitumia dhambi hii kwa kufanya mazuri. Kutokana na ukoo wa Daudi, Mungu alimleta Kristo katika ulimwengu.

Katika Agano la Kale, tunasoma kuhusu dhambi kuu sana. Waisraeli pamoja na Herode na Pilato na watu wa Mataifa wote walifanya kazi pamoja kumwua Mwana wa Mungu. Mwana wa Mungu alikuwa hana dhambi lakini walimwua. Walifanya dhambi kubwa sana. Lakini kwa mpango wa Mungu, hata hii ilikuwa kwa manufaa ya watu wake. "Huyu mtu akiisha kutolewa kwa shauri la Mungu tangu zamani, ninyi, kwa mikono ya watu wabaya, mlimwua kwa kumgongomea msalabani" (Matendo ya Mitume 2:23). Njia ambayo Kristo alisalitiwa na kuteswa na kusulubiwa yote haya yalifanyika kwa dhambi, lakini pia yote yalikuwa katika mpango wa Mungu.

Hii haimaanishi kwamba Mungu ndiye aliyewaongoza watu hawa katika dhambi wakati walipomsaliti Kristo na wakamwua. Watu hawa walitenda dhambi na walikuwa watenda dhambi. Lakini Mungu ndiye amedhibiti kila jambo na alitumia matendo yao kukamilisha mipango yake. "ni kweli Herode na Pontio Pilato pamoja na watu Mataifa na waisraeli, walikusanyika katika mji huu dhidi ya Mwanao Yesu uliyemtia mafuta. Wao wakafanya yale ambao uweza wako na mapenzi yako yalikuwa yamekusudia yatokee tangu zamani" (Matendo ya Mitume 4:27-28).

Dhambi kuu mtu anaweza kufanya ni kumchukia na kumwua Mwana wa Mungu. Lakini hata wakati watu walimchukia na kumwua Mwana wa Mungu, mapenzi ya Bwana yalifanikiwa mikononi mwake (Isaya 53:10). Nia ya Mungu ilikuwa kuangamiza dhambi kupitia kifo cha Kristo Yesu: "na kwa majeraha yake sisi tumepona" (Isaya 53:5). Hii ndiyo sababu Kristo Yesu alikuja. Alikuja kuonyesha kwamba Mungu ni mwenye nguvu zote na anaweza kugeuza dhambi kuu za wanadamu kufaidisha mipango yake. Ni mtenda dhambi ambaye alimwua Kristo na ni mtenda dhambi ambaye alifaidika kutokana na kifo cha Kristo Yesu kwa sababu Kristo aliomba, "Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo" (Luka 23:34).